**TRA** yavuka lengo Julai, yakusanya tril. 2.34/-



UKURASA 3

**Wadaiwa** kutumia picha, jina la Samia kutapeli

UKURASA 5



**AGNESS KAHAMBA;** Mwanadada Mtanzania anayeng'ara kimataifa

UKURASA 8


# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Agosti 11, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0581765

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US




**De Gea atua Fiorentina**

UKURASA 21

RIPOTI MAALUM

# Hatari wagonjwa wanaookatisha dozi

- **'Wachungaji',** waganga wa jadi wadaiwa chanzo, NIMR, matabibu waonya... *ukurasa 4*



Prof. Said Aboud



## Rais Samia akerwa na madudu ya Ushirika

UKURASA 2



## TLS yataka uchunguzi utekaji watu

UK. 3

MICHEZO YANGA, AZAM FAINALI YA AINA YAKE LEO UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

# Othman ahimiza matumizi fursa uchumi duniani

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema kuna umuhimu kwa Tanzania kuweka mkazo wa kutumia ipasavyo fursa za kiuchumi zilizoko katika nchi za Afrika Mashariki na mashirika mbalimbali ya kimataifa ili kusaidia nchi kukuza Uchumi.

Othman aliyasema hayo juzi ofisini kwake, Migombani, mjini Zanzibar, alipokutana na ujumbe wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ulioongozwa na Waziri, Balozi Mammoud Thibiti Kombo. Ujumbe huo ulifika ofisini kwa Othman kujitambulisha kutokana na mabadiliko ya hivi karibuni yaliyofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan.

Alisema kwa Tanzania, Afrika Mashariki si suala la uhusiano wa kijumuiya pekee bali ni fursa kubwa kiuchumi katika kuzitumia nchi za Kenya, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), Uganda na zingine katika shughuli mbalimbali za kibiashara na kiuchumi, mambo ambayo alisema zaidi ya ushirikiano katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC).

Makamu wa Rais alisema haja kubwa ya kujengwa uwelewa kwa wafanyabiashara na taasisi za serikali za Muungano na Zanzibar katika kuainisha na kuzitumia fursa za kiuchumi zilizoko katika maeneo hayo jambo litakalochangia kwenda sambamba na kasi ya kiuchumi duniani.

Alisema hatua hiyo ni pamoja na kuwawezesha wananchi kwa kuwajengea uwezo wa kuzitambua na kuzitumia fursa hizo ili kuwa na tija katika kusaidia kupunguza tatizo la ajira kwa wananchi wa pande mbili za Muungano.

Pia alisema hatua hiyo itasaidia Watanzania kumudu kwenda sambamba na kasi ya maendeleo hasa katika ulimwengu huu ambao kasi ya maendeleo ni kubwa sana.

Alizitaja baadhi ya taasisi za kimataifa kama vile Shirika la Haki Miliki (WIPO) lenye fursa kubwa za kiuchumi na kimaendeleo lakini Tanzania na Afrika kwa jumla inakosa uwakilishi, hivyo kupoteza fursa nyinngi ambazo ni muhimu katika kuchangia uchumi na maendeleo.

Othman alisema kuna haja kwa wizara hiyo kuhasmasisha makongamano ya kibishara na ushirikiano yatakayowezesha Zanzibar kutumiwa vyema fursa za kipekee zilizopo ambazo zinaweza kuinufaisha nchi kiuchumi.

Naye Waziri Kombo alisema watajitihadi kuyatumia maelekezo waliyopata kwa viongozi mbalimbali ambayo yatawasaidia katika kuelata tija kwa matumizi ya fursa zilizopo.

Alisema vita vya uchumi duniani vinashinda vya silaha na kwamba kuna haja ya kufanya kila aina ya jitihada za pamoja katika kuhakikisha taifa linasonga mbele.



Rais, Samia Suluhu Hassan, akizungumza na maofisa ugani pamoja na wanaushirika kabla ya kuanza kwa kikao na maofisa hao Ikulu Chamwino, Jijini Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

# Samia akerwa na madudu ushirika

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan ameeleza kukerwa na tabia ya baadhi ya viongozi wa vyama vya ushirika kujinufaisha na kuagiza vyama vya ushirika na ugani kutathmini matatizo yaliyoko na kuyapatia ufumbuzi kabla hajaondoka madarakani.

Samia alisema hayo jana Ikulu ya Chamwino, Dodoma, wakati akizungumza na maofisa ugani na maofisa ushirika kutoka halmashauri zote Tanzania Bara.

Alisema moja ya mambo ambayo yanamkera ni viongozi wa vyama vya ushirika kutumia vibaya nafasi zao kujinufaisha kupitia jasho la wakulima.

"Kazi ya ushirika ni kusimamia haki za wanaushirika, lakini imekuwa sivyo viongozi wengi wanatumia nafasi zao kujinufaisha wao binafsi, badala ya wakulima walitumia nguvu zao kulima mazao yao," alisema. Rais Samia alisema vitendo hivyo vinavyofanywa na viongozi wa ushirika nchini ni dhambi kubwa.

"Leo mkulima kalima na kavuna lakini kiongozi ndiye anakuwa mnufaika wa mazao yale ambayo mkulima ametoa jasho lake. Ni dhambi kubwa sana. Kazi ya ushirika inapaswa kuwa ni kulinda maslahi ya wakulima, badala ya kuwa viongozi ndiyo wa kwanza kuminya haki za wanaushirika wao," alisema.

Kutokana na hali hiyo, Rais Samia alisema anataka kuona hali hiyo inabadilika ili ushirika uwe mtetezi wa wakulima, badala ya viongozi kuutumia kujinufaisha binafsi.

"Ninaomba matatizo yenu yote ambayo yamekuwapo mjitathmini na tuone nini cha kufanya ili kuyamaliza kabla muda wangu wa kuelekea Kizimkazi mwaka 2029,"alisema.

Rais Samia aliiagiza Wizara ya Kilimo kuhakikisha inatekeleza maagizo yake ya kuanzishwa kwa wakala wa huduma za ugani nchini.

"Wakala huu utumike kusimamia huduma za ugani nchini, lakini pia kutumika kwa ajili ya kuwapima wagani kwa huduma wanazo zitoa kwa wakulima,"alisema.

Rais Samia aliahidi kutoa Sh. bilioni tano kwa ajili ya kuchangia kuanzishwa kwa Benki ya Taifa ya Ushirika itakayosaidia kuimarisha vyama ushirika nchini na kuongeza tija kwa wanachama wake.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, alisema serikali imeendeleza jitihada zake za kuwezesha sekta hiyo katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita.

Alisema jitihada hizo ni pamoja na kurudisha chanjo ya mifugo ya taifa ya mifugo ambayo iliondolewa kwa muda mrefu nchini.

"Ndani ya utawala wako, Mheshimiwa Rais umefanya mambo mengi sana katika sekta ya mifugo na uvuvi ikiwamo katika mwaka huu wa fedha, umetenga kiasi cha Sh. bilioni 28, kwa ajili ya kurejesha chanjo ya mifugo ya taifa, ambayo itasaidia wafugaji kuchanja mifugo yao,"alisema.

Ulega alisema serikali pia, imetoa mafunzo rejea ya teknolojia na maarifa mbalimbali kwa maofisa ugani 3,600 ambapo kati yao 3,100 ni wa mifugo na 500 wa uvuvi.

Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alisema serikali imewekeza fedha nyingi katika kilimo katika kipindi hiki cha miaka mitatu zikitumika pia katika ununuzi wa vifaa kwa ajili ya maofisa kilimo.

Pia alisema katika fedha hizo serikali imenunua magari , vifaa vya kisasa vya kupima udongo pamoja na pikipiki ambazo zimefungwa kifaa maalum cha kutambua ziliko.

# Bunge laita wadau maoni miswada ya sheria

**Na Beatrice Shayo**

KAMATI nne za Kudumu za Bunge zimewaalika wadau kutoa maoni kuhusu miswada minane ya sheria ukiwano Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Hifadhi za Jamii wa Mwaka 2024.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana kwa vyombo vya habari na Kitengo za Mawasiliano na Uhusiano wa Kimataifa, Ofisi ya Bunge, maoni hayo yataanza kupokewa kuanzia Agosti 14 hadi 16, mwaka huu.

Taarifa hiyo ilisema Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria itapokea maoni kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Shule ya Sheria Tanzania wa mwaka 2014 (The Law School of Tanzania).

Mingine ni Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali wa Mwaka 2024, Muswada wa Sheria ya Marekebisho mbalimbali (Na.2) wa Mwaka 2024 na Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa wa mwaka 2024.

Aidha, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii itapokea maoni kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Hifadhi ya Jamii wa Mwaka 2024 na Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria zinazohusu Ulinzi wa Watoto.

Taarifa hiyo ilisema kuwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo itapokea maoni ya Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ushindani wa Haki wa Mwaka 2024.

Kadhalika, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu itapokea maoni ya Muswada wa Sheria ya Viwanja vya Ndege Tanzania wa Mwaka 2024.

Taarifa hiyo ilisema kuwa kamati zitapokea na kusikiliza maoni ya wadau kuanzia saa 4:00 asubuhi Agosti 15 hadi 16, mwaka huu.

Pia taarifa ilisema Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria itapokea maoni ukumbi wa Frank Mfundo, jengo la utawala Ofisi ya Bunge jijini Dodoma.

Taarifa hiyo ilisema Kamati ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii itapokea maoni Agosti 15 na 16, mwaka huu, katika ukumbi wa Pius Msekwa, Ofisi ya Bunge, jijini humo.

"Agosti 14, mwaka huu, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo itakutana katika ukumbi wa Msekwa D, jengo la Pius Msekwa, Ofisi ya Bunge Dodoma.

"Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu itakutana katika ukumbi namba 231, jengo la utawala Ofisi ya Bunge," ilisema.

Taarifa hiyo ilisema maoni yanaweza pia, kuwasilishwa kwa njia ya posta kupitia anuani ya Ofisi ya Bunge au kupitia barua pepe za cna@bunge.go.tz na kamati@bunge.go.tz.

## HABARI KITAIFA

## TRA yavuka lengo Julai, yakusanya tril. 2.34/-

**Na Beatrice Shayo**

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) imekusanya Sh. trilioni 2.34 kwa mwezi Julai ikiwa ni zaidi ya lengo lililowekwa kwa asilimia 104.4 kulinganisha na lengo la Sh. trilioni 2.246.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana kwa vyombo vya Habari, iliyotiwa saini na Kamishna Mkuu wa TRA, Yusuph Mwenda, makusanyo hayo ni sawa na ukuaji wa asilimia 20.9 ikilinganishwa na Sh. trilioni 1.94 zilizokusanywa Julai, mwaka jana, kwa mwaka wa fedha 2023/24.

Alisema ufanisi katika makusanyo na ukuaji wa makusanyo kwa Julai, mwaka huu, ni wa kiwango cha juu kufikiwa na TRA katika kipindi cha miezi sita iliyopita.

Mwenda alisema ufanisi huo umechangiwa na kuboresha uhusiano kati ya mamlaka na walipakodi kwa njia za mawasiliano na majadiliano.

Pia alisema hatua hiyo ni kutokana na kuchukua hatua za haraka katika vihatarishi vya ulipaji kodi pamoja na vitendo vya ukwepaji wa kodi.

Mwenda pia alisema kuongezeka kwa usimamizi wa watumishi wa TRA na kuendelea kuwapatia mafunzo kwa vitendo watumishi wapya kwa lengo la kuongeza uadilifu na weledi katika utendaji wao wa kazi.

Alisema wameongeza usimamizi wa matumizi sahihi ya Mashine za Kieletroniki (EFD) na matumizi ya Stempu za Ushuru wa Bidhaa (ETS). Ufanisi wa makusanyo uliofikiwa na TRA kwa mwezi Julai, alisema ni kiashiria chanya katika kuhakikisha lengo la makusanyo kwa mwaka huu wa fedha la Sh. trilioni 30.4 linafikiwa.

Katika kufanikisha jambo hilo, alisema menejimenti ya TRA imejipanga kutekeleza mambo 12 ikiwamo maagizo yote yaliyotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan, kuhusu usimamizi wa kodi.

Mwenda alisema hali hiyo pia imetokana na kuimarisha uhusiano na ushirikiano na walipakodi pamoja na wananchi wote, kuimarisha utoaji wa elimu ya kodi na huduma bora kwa walipakodi na kujenga na kuimarisha mifumo ya kodi za ndani na forodha. "Kusimamia na kuimarisha misingi ya mfumo mzuri wa kodi ikiwamo haki na usawa katika utozaji kodi (No Favouritism or Victimization)," alisema.

Mwenda alisema mamlaka itaimarisha na kusimamia weledi taaluma yao na huduma nzuri kwa walipakodi ikiwamo watumishi wao wote kuvaa vitambulisho wanapotoa huduma ili kuweka uwazi baina ya mtoa na mpokea huduma.

Aidha, alisema watasikiliza na kutatua changamoto za kikodi za walipakodi kwa wakati nchi nzima.

"Kushirikiana na Tume ya Rais ya Tathimini ya Mfumo wa Kikodi Nchi ni ili kuwa na mfumo rafiki unaosimamia usawa, unaorahisisha shughuli za kiuchumi na wenye tija nchini," alisema.




RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akikabidhiwa Tuzo Maalum kwa Mchango wake kwa Vijana na Mwasisi wa Taasisi ya Global Youth Empowerment, Amina Sanga, baada ya kufungua Kongamano la Kitaifa la Kuwawezesha Vijana, lililofanyika katika ukumbi wa Hoteli ya Zanzibar Beach Resort, Mazizini Zanzibar. **PICHA: IKULU**

# TLS yataka uchunguzi utekaji watu

**Na Romana Mallya**

CHAMA cha Wanasheria Tanganyika (TLS) kimemshauri Rais Samia Suluhu Hassan, kuunda tume maalumu ya kuchunguza matukio yote ya kudaiwa kupotea kwa watu, kutekwa na kuteswa.

Pia kimemshauri Rais Samia kuunda tume maalum ya kuchunguza ushiriki wa Jeshi la Polisi katika masuala ya utekaji kwa inachodai kuwa jeshi hilo limekuwa likituhumiwa kushiriki katika vitendo hivyo. Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na juzi na Rais wa TLS, Boniface Mwabukusi, chama kinasikitishwa na kinalaani vitendo vya kukamatwa, kutekwa na kuteswa kiholela kwa wananchi kunakoendelea nchini bila ya vyombo husika vya dola kuwajibika ipasavyo.

"Kumekuwapo na taarifa mbalimbali za watu kupotea katika mazingira tatanishi, kutekwa na kuteswa na baadaye kuonekana, huku baadhi yao wakiwa wamefariki dunia na wengine wakiwa na majeraha makubwa katika miili yao.

"Tunasikitishwa pia na namna ambavyo vyombo vyetu vya dola hususani Jeshi la Polisi limekuwa likifanyia kazi taarifa hizo. Mara kwa mara Jeshi la Polisi limekuwa likikanusha kutokea kwa matukio hayo, lakini baadaye inakuja kubainika kwamba, matukio hayo ni ya kweli," alidai Mwabugusi.

Kutokana na matukio hayo, TLS imependekeza kuundwa kwa chombo maalumu cha kudumu cha kuangalia utendaji wa vyombo vya dola ili kuhakikisha vinafanya kazi kwa mujibu wa katiba na sheria.

"Tunalitaka Jeshi la Polisi kufanya kazi yake kwa weledi kwa mujibu wa katiba na sheria ili kuhakikisha usalama na ulinzi wa wananchi na mali zao unaimarika.

"TLS inaendelea kufuatilia matukio haya kwa ukaribu na iko tayari kushirikiana na vyombo vyote vya dola katika kuhakikisha wahusika wote wa matukio haya wanafikishwa katika vyombo mahususi vya haki ili haki ionekane inatendeka," alisema.

Mwabugusi alisema TLS inatoa rai kwa watanzania wote kuwa makini wakati wote na kutokubali kuitwa au kukutana na watu wasiowajua au kwenda mahali wasipopajua na ikibidi wawasiliane na wakili yeyote kabla ya kukutana au kwenda mahali wasipopajua.

Katika taarifa yao, TLS imedai mara nyingine Jeshi la Polisi limekuwa likiwakamata raia wema wanaotoa taarifa hizo kwa kile kinachosemekana kusambaza taarifa za uongo badala ya kufanyia kazi taarifa hizo kwa mujibu wa Katiba na sheria zinazowapasa kufanya wajibu wao wa kulinda watu na mali zao. "TLS kwa mamlaka iliyopewa kupitia kifungu cha 4 cha Sheria iliyounda TLS (Tanganyika Law Society Act, Cap. 307 R.E. 2002), inapenda kuvikumbusha vyombo vya dola hususan Jeshi la Polisi kuhusu majukumu yake ya kikatiba na kisheria ya kulinda watu na mali zao," alisema.

Mwabugusi alisema matukio hayo ni kinyume na Ibara ya 13 (6) (e) na 14 ya Katiba; pamoja na mikataba ya kimataifa inayozungumzia haki za binadamu na inayozuia uteswaji wa watu kama vile Mkataba dhidi ya mateso na unyanyasaji au adhabu nyingine za kikatili au udhalilishaji. "Kinyume cha Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu na Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa. TLS inatambua na kuheshimu taarifa za Jeshi la Polisi zinatolewa zikitaarifu umma kwamba, matukio hayo yamekuwa yanafanyiwa uchunguzi.

"Lakini tunasikitika kwamba hakuna taarifa kamili ya uchunguzi wa tukio hata moja ambayo imewahi kutolewa kwa umma kuhusu hatua zilizochukuliwa na Jeshi la Polisi juu ya watuhumiwa wa matukio hayo," alisema. Mwabugusi alisema hali hiyo inaendelea kutia hofu kwa wananchi kuhusu usalama wao na mashaka ya uwezo wa Jeshi la Polisi kuchunguza na kuchukua hatua stahiki kwa wahusika wa matukio hayo.

"Kupitia tamko hili, tunaambatanisha orodha ya baadhi ya watu ambao wananchi au na vyombo mbalimbali vya habari hapa nchini vimewahi kutoa taarifa za kupotea au kutekwa kwao. Baadhi yao walipatikana na baadhi yao wakiwa na majeraha huku kukiwa na wengine ambao waliopotea katika mazingira tatanishi na hawajapatikana mpaka leo," alisema.

Katika taarifa hiyo, TLS imetaja watu 83 wanaodaiwa kutekwa au kupotea kwa miaka minane kuanzia mwaka 2016 hadi 2024.

Waliodaiwa kutekwa na baadhi kupatikana waliowataja ni pamoja na Ben Saanane (Dar), Azory Gwanda (Pwani), Simon Kanguye (Kigoma) na Joshua (Iringa).

Wengine Kombo Twaha (Handeni-Tanga), Kennedy Mwamlima mkazi wa Mbeya Edger Mwakalebela (Dar), James Sije (Nyakato-Mwanza), Joseph Mnyonga (Mwanza), Dotto Kabwa (Ifunga-Iringa) na Yahya Ally (Dar). Chande Kizega (Dar), Mzee Samuel Mkongo (Geita Mjini), Charles Mwampyate (Dar), William Herman (Kangaye-Mwanza), David Lema (Mwanza), Jerome Kisoka (Kilimanjaro) na Ridhiwani Msangi (Iringa).

Benson Ishungisa (Dar), Hamza Said (Mwatulole-Geita), Yonzo Dutu (Kishapu-Shinyanga), Lilenga Isaya (Mwandiga-Kigoma), Tawafiq Mohamed (Dar), Self Swala (Dar), Edwin Kunambi (Dar), Hemed Abass (Dar), Maseke Mwita (Mara) na Rajab Mdoe (Dar).

Wengine ni Mzee Haji Soft (Dar), Alphonce Bilasenge (Kagera), Albert Selembo na Moloimeti Saing'eu, Ndirango lazier, Joel Lessonu, Simoni Orosikiria, Damian Laizer, Mathew Siloma na Lukas Njausi. Taleng'o Leshoko, Kijoolu Olojiloji, Shengena Killel, Malongo Paschal, Simeli Korongoi, Ingoi Kanjwei, Sangau Ngiminis, Marijoi Parmati, Morongeti Masako, Kambatai Lulu na Orias Oleng'iyo.

Wilson Kolong, James Taki, Joseph Jartan, Kelvin Nairoti, Lekerenga Orodo, Fred Ledidi, Simon Morintanti wote kutoka Loliondo, mkoani Arusha. Wengine ni Mohamed Kalebe (Geita), Amon Magige (Mwanza), Aziz Kinyonga na Yusuph Dudu kutoka Dar es Salaam, Kastory Kapinga (Mbinga), Dioniz Kipanya (Rukwa), Shadrack Chaula (Mbeya) na Prosiper Mnjari (Dar).

Pia wamo Thomas Ihuya (Mwanza), Dennis Kantanga (Shinyanga), Damas Bulimbe na Lucas Bulimbe (Geita), Matuki Makuru (Mara), Dastan Nestory na Adinan Mbezi wote kutoka Geita. Lengaripo Lukumay (Mwanza), Akidu Salim (Dar), Enock Chambala (Tanga), Dioniz Kipanya (Katavi), Nusra Omari (Dar), Theresphora Mwakalinga (Dodoma), Donald Mboya (Kagera), Ilham Makoye, Barack Majigeh, Yusra Musa, Angel Kamugisha, Brighton Emmanuel wote kutoka Dar.

Mwabukusi alisema wanaamini Jeshi la Polisi na vyombo vingine vya dola vitafanyia kazi na kuhakikisha watu hao wamepatikana na wahusika wote wa matukio hayo wanakamatwa na kufikishwa katika vyombo husika vya haki ili hatua stahiki za kisheria ziweze kuchukuliwa.

# Hatari wagonjwa wanaokatisha dozi

## -‘Wachungaji’, waganga wa jadi wadaiwa chanzo, NIMR, wataalamu tiba waonya

**Na Waandishi Wetu**

HILI ni janga linalowanyemelea wagonjwa wengi wanaougua magonjwa mbalimbali, yakiwamo sugu kwa kukatiza dozi wanapoona wana unafuu.

Wataalam wa afya, wakiwamo madaktari, wamebainisha suala hilo lipo katika jamii na husababisha madhara vikiwamo vifo huku wakiwatupia lawama baadhi ya viongozi wa dini wanaowaombea na waganga wa kienyeji kuwa sehemu ya chanzo cha kuwapo hali hiyo.

Kwa mujibu wa matabibu hao, wagonjwa huacha dozi kwa kuambiwa watapona baada ya kufanyiwa maombi, huku waganga wa kienyeji wakidaiwa kushawishi kuacha dawa walizopewa na wataalam wa afya na kuwataka watumie dawa za asili.

Daktari Bingwa kutoka Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Benjamin Mkapa (BMH) jijini Dodoma, Dk. Joshua Youze, anasema kutokumaliza dozi hususan kwa wagonjwa wanaougua maradhi mbalimbali, yakiwamo sugu, kunachangia kuleta fangasi na kuongeza tatizo la usugu mwilini.

Anasema moja ya tatizo sugu linaloweza kupatikana kwa mgonjwa aliyeacha dozi ni pamoja na mgonjwa kupata fungasi akiwa na ugonjwa ngozi.

Dk. Youze anasema mgonjwa wa aina hiyo akirejeshwa tena hospitalini inabidi abadilishiwe dozi na kupewa nyingine kali ili ugonjwa wake upone. Anasema baada ya uchunguzi kufanyika, wamebaini suala baadhi ya watumishi wa Mungu kulingana na imani zao za dini ni chanzo kikubwa cha wagonjwa kuacha dozi wanazopewa.

“Hili suala linatuumiza sana madaktari, tunaomba serikali iliangalie suala hili. Dini haikatazwi lakini wasimwaribie dozi mgonjwa aliyeenda katika maombi,” anasema Dk. Youze.

Pia anasema imani za kishirikina nazo huchangia kwa kiasi kikubwa wagonjwa kukatisha dozi wanazopewa na madaktari, hivyo kuiomba kuingilia kati baadhi ya madhehebu ya dini ambayo huchangia wagonjwa kutupa dawa na kuendelea na maombi kitu ambacho siyo sahihi wanatakiwa kuwa na mipaka.

Anasema hakuna mtu asiyesali wala kuomba, lakini inapofika suala la tiba ni lazima ingatiwe ili dawa zilete uponyaji.

Anasema kinachopaswa kufanyika ni pamoja na jamii kujengewa uwezo wa umuhimu wa kutumia dawa pamoja na kupewa elimu kuhusu madhara ya kuachilia dozi ili hali unaumwa.

Anafafanua kuwa kitendo cha viongozi wa baadhi ya madhehebu ya dini kuwakataza wagonjwa wasitumie dawa ili waendelee na maombi ni kuingilia kazi za madaktari.



Jambo hilo limeungwa mkono na Mchungaji wa Kanisa la Kiinjili na Kilutheri Tanzania (KKKT), Dk. Enock Mlyuka, ambaye anasema baadhi ya watu wanaojiita watumishi wa Mungu wanafanya huduma wanazofanya kwa kisingizio ni huduma ya Mungu.

“Lengo ni kutumia matatizo ya watu kujinufaisha na ili afanikiwe lazima afanye mambo ya kuvutia watu wamuone ni mtu wa pekee.“Hayo mambo yanayofanywa na baadhi ya watu wanaojiita watumishi wa Mungu ni pamoja na kufanya matendo yanayoonekana ni ya kiroho, kama miujiza na kwa kuwa watu wengi wana matatizo na wanapenda miujiza watakwenda.

“Hao wanaojiita watumishi wa Mungu ni kama hawaamini kwamba, Mungu amegawa vipawa, ujuzi na maarifa kwa watu mbalimbali na huo ujuzi na maarifa unatoka kwa Mungu kusaidia jamii. Mfano madaktari na wauguzi hospitalini, ile ni huduma ya Mungu,” anasema.

Dk. Mlyuka anasema watu hao ili kuonekana ni wa pekee, wanachofanya ni kuonesha kule (hospitalini) sio ila huduma zao ndio.

“Na mtu anapokwenda kwao akiwa na matatizo ambayo yatahitaji wataalam wa afya, watambia usiende kule utapata huduma ya uponyaji hapa na mwishoe huishia kufa. Huo ni utapeli wa kiroho na haukubaliki na wanachafua kada ya utumishi wa Mungu,” anasema.

### HOLELA HOLELA ITAKUKOSTI

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR), Prof. Said Aboud, anasema kuna utafiti mbalimbali uliofanyika kuhusu Usugu wa Vimelea vya Dawa za Antibiotiki (UVIDA).

“Matokeo ya utafiti huo ni kuongezeka kwa UVIDA, kutopona ugonjwa unaotibiwa, kusababisha kifo, kuongezeka kwa muda wa kukaa hospitalini kwa ajili ya kupatiwa matibabu.

“Usitumie dawa yoyote bila ya cheti cha daktari. Kuna kampeni inayoendelea ya kuelimisha wananchi kuhusu UVIDA, inaitwa ‘holela holela itakukosti,’” alisema.

### HUCHANGIA VIFO

Mratibu wa Kifua Kikuu Halmashauri ya Wilaya ya Meru, mkoani Arusha, Dk. George Marwa, anasema mgonjwa anapoandikiwa dozi na kutomaliza, kuna uwezekano mkubwa wa kutokupona na kufariki dunia.

Anasema sababu ya pili ni pamoja na vimelea vya ugonjwa kuwa sugu na kutokusikia dawa, huku akitolea mfano wa mtu mwenye Virusi Vya UKIMWI (VVU) ambaye huchangia virusi kushamiri na kutosikia dawa pale anapokatisha dozi ya Kifua Kikuu (TB) na anapobainika kuwa nayo.

“Athari ni nyingi na kwa sababu hiyo ni lazima watu wazingatie kumaliza dozi wanazoandikiwa ili kukomesha usugu, kurudiwa na ugonjwa au wakati mwingine kupelekea kifo,” anasema Dk. Marwa.

Daktari Jimmy Julius wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Tanga - Bombo, anasema kutokumaliza dozi huchangia vimelea vya wadudu kuendelea kuwapo mwilini kutokana na kutokupata tiba sahihi.

Dk. Julius anasema kwa kufanya hivyo huchangia mgonjwa kutumia gharama kubwa zaidi katika kupata matibabu, hivyo kushauri kuzingatia maelekezo ya wataalam wa afya.

Naye Daktari wa Magonjwa ya Afya ya Akili hospitalini hapo, Dk. Wallace Karata, anasema kutomaliza dozi ambayo mgonjwa ameandikiwa husababisha usugu wa dawa mwilini.

Daktari wa Kitengo cha Upasuaji kutoka Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Manyara, Dk. Ludovick Legama, anasema wagonjwa ambao hawamalizi dawa wanazoandikiwa huwa hawaponi na wanaharibu soko la dawa husika na kuwapa nguvu bakteria ya kuendelea kuishi mwilini.

“Bakteria huwa wanaweza kujipanga namna ya kuharibu hiyo dawa kwa kuwa ukiacha dawa wanatengeneza mazingira ya kuikwepa ili isiwadhuru.

“Wale wadudu tukipandikiza na bakteria 10 baada ya siku saba, tunakuta wapo 20 tunajua wamezaliana baada ya hapo tunawawekea dawa kuona kama wamekufa, na iwapo wamekufa tunajua dawa imefanya kazi au kama hawajafa tunajua wamejenga usugu,” anasema.

Daktari kutoka Hospitali ya Rufani ya Kanda KCMC, Dk. Ebenezer Mary, anasema kwa sasa kumekuwa na matatizo ya umezaji wa dawa bila kufuata maelekezo ya matatibu, hali inayochangia matatizo hasa ya usugu wa dawa.

‘Ingawa sina takwimu kamili ila hali ni mbaya kwa jamii, watu wengi hutumia dawa na kukatisha dozi na wengine kutumia dawa kwa hisia wanaumwa ugonjwa fulani, hii inapaswa kukemewa na jamii kuelimishwa kutokana na madhara yanayoweza kutokea,”anasema Dk. Maro.

Aidha, anawataka wanasiasa kutumia muda mingi kuelimisha wananchi kwa lengo la kukuza jamii yenye afya bora.

Mganga Mfawidhi Kituo cha Afya Igalla, Ukerewe mkoani Mwanza, Dk. Jeremia Katwale, anasema wagonjwa wengi hasa wa Malaria hawamalizi dozi kwa sababu ya harufu ya dawa, wingi wa vidonge na siku za kumeza kuwa nyingi, hivyo wakiona wana nafuu huikatisha.

“Dozi ya Malaria ukimeza ya kwanza na dozi ya pili inatibu kwa asilimia 90 na hizo dozi zilizobaki ndio zinamalizia asilimia 10 iliyobaki, ndiyo maana mtumiaji akimeza dozi ya pili unakuta amepata unafuu na kuona hakuna haja ya kumalizia,” anasema.

Dk. Katwale anasema kuwa athari zinazoweza kupatikana ni usugu wa dawa ambapo mgonjwa akipatwa na ugonjwa, dawa aliyoitumia mwanzo inaweza isimtibu.

Anasema changamoto nyingine ni baadhi ya wagonjwa kuwa na Imani na miti shamba wakati ugonjwa alionao mfano Malaria unapaswa kutibika na dawa za hospitalini.

**• IMEANDALIWA na Romana Mallya (DAR), Renatha Msungu (DODOMA), Jaliwason Jasson (MANYARA), Tumaini Mafie (ARUSHA), Mary Mosha (MOSHI), Assenga Oscar (Tanga) na Neema Emmanuel, (MWANZA)**

HABARI KITAIFA

# Kampuni yadaiwa kutapeli vijana kwa kutumia jina la Rais Samia

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

ZAIDI ya vijana 500 kutoka mikoa mbalimbali nchini, wamedaiwa kutapeliwa na kampuni ya Alliance in Motion Global ya Kahama mkoani Shinyanga, kwa kutumia jina la Rais Samia Suluhu Hassan.

Kampuni hiyo imekuwa ikijitangaza na kuwalaghai vijana kupitia mabango kuwa itawapatia mafunzo na ajira.

Aidha, inadaiwa kushikilia nyaraka mbalimbali muhimu za vijana hao vikiwamo vyeti vya elimu ya sekondari, vya kuzaliwa, vitambulisho vya taifa (NIDA) na vya mpigakura, ili kuwashinikiza kulipa fedha zinazodaiwa kutumika katika malazi na chakula na kulala chumba kimoja kwa vijana sita.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita, alibainisha hayo jana baada ya kufanya ziara ya kushtukiza katika ofisi za kampuni hiyo zilizoko katika kata za Mhongolo, Malunga-Igomelo na Nyihogo Halmashauri ya Manispaa ya Kahama.

Mhita alisema wote waliohusika kuwatapeli watawajibishwa kisheria ili iwe fundisho kwa kampuni zenye tabia kama hizo.

Alisema ofisi yake ilipokea malalamiko ya vijana hao kuhusu kutapeliwa na kampuni hiyo kwa kuchukuliwa fedha zao kwa kigezo cha kupewa mafunzo na ajira katika kampuni na viwanda mbalimbali.

Baada ya kupata taarifa hizo, alisema alichukua hatua ili kufuatilia uhalali wa kampuni hiyo kushirikiana na kamati ya usalama na kubaini vijana hao kutapeliwa.

Mhita alisema kampuni hiyo ina vijana ambao inawatumia kuwatafuta ndugu, rafiki na jamaa wa karibu kwa kulaghai kwa kuwatoza fedha na kuwa wengepata ajira kwa kulipwa ujira wa Sh.350,000 mpaka 500,000.

Mkuu wa wilaya alisema vijana wengi waliotoa taarifa hizo ni wale ambao waligundua kuwa wametapeliwa baada ya kuona muda unakwenda bila kuwapo dalili zozote za ajira.

"Sihitaji kuona kampuni hii ikiendelea kufanya kazi wilayani hapa tena kwa kutumia picha na jina la Rais Samia Suluhu Hassan kuwaaminisha vijana na kuwatapeli fedha ambazo wangezitumia kujiendeleza kiuchumi kupitia ujasiriamali kwenye maeneo wanayotoka na kuondokana na utegemezi," alisema.

Mhita aliwataka viongozi wa kampuni hiyo kurejesha nyaraka muhimu za vijana hao vikiwamo vyeti vyao vya elimu na fedha walizotoa kulipia mafunzo, malazi na chakula.

Pia alisema wale waliowapangisha makazi kampuni, watalisaidia Jeshi la Polisi kuwabaini ili iwe fundisho kwa wengine wanaotapeli vijana.

Mkazi wa Wilaya ya Kasulu mkoani Kigoma, William James, alisema alipigiwa simu na rafiki yake na kumweleza kuwa kuna kazi katika kiwanda cha kuchakata mazao ya samaki na alipofika, aliombwa Sh. 120,000 zikiwamo Sh. 20,000 za gharama za fomu ya kujinga na 100,000 mafunzo, kulala na chakula lakini mpaka sasa hajapata kazi hiyo.

Naye Method Waziri, kutoka mkoa wa Pwani, alisema alidanganywa kuwa kuna kazi na mshahara ni Sh.350,000. Alisema alipofika alikuta wanafundishwa masuala ya afya kwa maana ya kufunga dawa za asili, kutafuta wateja na kupaki kwenye vifungashio.

"Awali, niliamini kampuni hii baada ya kuona picha ya Rais Samia ikiwa kwenye mapango yao na ujumbe usemao 'Ahsante Rais kwa kutujenga vijana kuchangamkia fursa pasipo kutegemea ajira'," alisema Jasmini Jabili kutoka mkoani Kagera

Msimamizi wa kampuni hiyo, Shafii Jumanne, alikiri kuwapo kwa vijana hao ambao wanawapatia elimu ya afya ya utengenezaji na ufungaji wa bidhaa na uchumi na wengi wanatoka mikoa mbalimbali nchini kwa sababu kampuni hiyo inafanya kazi mikoa yote na inalipa kodi serikalini.

Alisema hawezi kujua kama fedha zilizotolewa zinaweza kurejeshwa kwa vijana hao isipokuwa nyaraka mbalimbali walizozichukua vikiwamo vyeti na kwamba atawasiliana na mamlaka za juu ili kuvirejesha na kukubali kufunga ofisi hiyo isiendelee kufanya kazi mpaka pale serikali itakapotoa uamuzi mwingine dhidi yao.



Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, akizungumza katika hafla ya ufungishaji wa ndoa 100, zilizofadhiliwa na taasisi ya Al-hikma Foundation jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Wahamiaji haramu 13 wadakwa, wakutwa hoi kwa kukosa chakula

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

JESHI la Polisi mkoani Shinyanga linawashikilia wahamiaji haramu 13 kutoka Ethiopia, huku 11 kati yao wakikutwa hoi kwa kukoswa chakula, hivyo kulazwa katika Hospitali ya Manispaa ya Shinyanga.

Watu hao walitekelezwa kwenye pango katika kijiji cha Wishiteleja wilayani Kishapu mkoani hapa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Janeth Magomi, alisema wahamiaji hao waliwakamata Agosti 8, mwaka huu, majira ya saa 12:00 jioni baada ya kupewa taarifa na raia wema na kuwakuta wakiwa katika hali mbaya kutokana na kukosa chakula.

"Walikuwa wamejificha katika pango na tulikuta mikate ikiwa imeoza pamoja na maji, ikimaanisha kwamba walikuwa wakiishi kwa kunywa maji na kula mikate. Hali zao kiafya zilikuwa mbaya sana," alisema Magomi.

Kamanda Magomi alisema wahamiaji hao 11 bado wanaendelea kupatiwa matibabu na hali zao kiafya zinaendelea kuimarika, huku wawili wakiwakabidhi idara ya uhamiaji kwa ajili ya taratibu zingine za kisheria.

Alisema jeshi hilo bado linaendelea na uchunguzi ili kubaini mtu ambaye amewaletea wahamiaji hao haramu na kwamba hawawezi kuingia nchini Tanzania bila kuwa na mwenyeji. Alitoa wito kwa wananchi kuendelea kutoa taarifa za wahalifu na wahamiaji haramu. Mmoja wa wahamiaji hao, Maratha Rapson, akizungumza akiwa hospitalini, alisema walikuwa wanatoka Ethiopia wakienda Afrika kusini kutafuta kazi.

# Washauri wakuu wa shule kuanzisha klabu za fedha mashuleni

**Na Mwandishi Wetu,** LINDI

SERIKALI imeshauriwa kuwasimamia wakuu wa shule kuongeza kasi ya kuanzisha klabu za mambo mbalimbali yakiwamo ya fedha katika shule ili zitumike kutoa elimu hiyo na mambo mengine ya kijamii.

Ushauri huo ulitolewa juzi na Mlezi wa Klabu katika Shule ya Sekondari ya Kutwa Liwale, Mwalimu Mustafa Likambako, alipokutana na timu ya wataalamu kutoka Wizara ya Fedha ambayo iko mkoani hapa kutoa elimu ya masuala ya fedha kwa makundi mbalimbali ya wananchi wakiwamo wanafunzi, wafanyabiashara, wakufunzi na wajasiriamali.

"Katika shule yetu tuna klabu tatu za mazingira, masuala ya rushwa na femina. Kwa kuwa mimi ndiye mlezi wa klabu hizo, nimeona zinavyowasaidia wanafunzi kuwa na uelewa mpana wa masuala ya kijamii wanayojifunza muda wa ziada," alisema.

Alisema kuna umuhimu kwa Wizara ya Fedha kuanzisha klabu ya masuala ya fedha katika shule mbalimbali ili wanafunzi wafundishwe matumizi ya fedha tangu wakiwa wadogo ili wakiwa wakubwa wawe na uelewa wa masuala hayo.

"Shuleni kwetu tuna matamasha ambayo huwa tunatumia jukwaa hilo kuwashindanisha wanafunzi wa klabu mbalimbali na kutoa zawadi. Hii inasaidia kumfanya mwanafunzi awe makini darasani lakini kuwa na juhudi binafsi yakusoma na kushika wanachofundishwa", alisema Likambako.

Alisema iwapo zitaanzishwa klabu za masuala ya fedha katika shule itasaidia kupata mabalozi ambao ni wanafunzi na wakirudi nyumbani likizo wanakuwa walimu wazuri kwa wazazi na jamii inayowazunguka

Naye Ofisa Mchambuzi Hesabu Mwandamizi kutoka Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA), Mariam Mtunguja, alisema wametoa elimu ya masuala ya fedha kwa makundi mbalimbali wakiwamo wanafunzi, wakufunzi, vikundi vya wajasiriamali na wafanyabiashara.

"Tumeona kiu ya wanafunzi kuuliza maswali mengi wakitaka kujua mitaji inatakiwa kuanzia shilingi ngapi, lakini waliuliza kama wanafunzi wanaruhusiwa kuwa wawekezaji nimeona kuna umuhimu wa elimu hii kuanza kutolewa mapema katika shule mbalimbali", alisema Mtunguja.

Mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Liwale Day, Zuleikha Hamidu, aliahidi kuanza kuweka akiba kwenye fedha za matumizi anazopewa na wazazi wake ili kumsaidia kwa baadaye.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kwa hatua hii ya TRA, malalamiko ya wafanyabiashara yatapata jawabu

**KWA** muda mrefu kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wafanyabiashara kuhusu masuala mbalimbali kutoka kwa watumishui wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) miongoni mwa malalamiko hayo ni madai ya kubambikiwa kodi, watumishi wa mamlaka hiyo kuwaomba rushwa wafanyabiashara huku wakiwatishia kuwafikisha kwenye vyombo vya sheria kuwa wanakwepa kodi na matumizi ya nguvu katika kudai kodi.

Katika miaka ya karibuni kwa mfano, baadhi ya wafanyabiashara walilalamika mbele ya viongozi wakuu wa serikali kwamba baadhi ya wafanyakazi wasio waaminifu wa TRA wamekuwa wakichukua mizigo yao kwa nguvu na kuificha kusikojulikana, hali ambayo huwasababishia hasara.

Hali hiyo ilizidi kuwa mbaya hivi karibuni baada ya wafanyabiashara kufunga maduka yao kwa madai kama hayo kuwa wananyanyaswa na maofisa wa TRA ambao wamekuwa wakiwabambikia kodi au kufanya makadirio ya juu tofauti na thamani ya bidhaa. Hatua hiyo ilisababisha si tu wafanyabiashara kupata hasara bali serikali kukosa mapato ikizingatiwa kwamba sehemu kubwa ya mapato ya serikali ambayo ndiyo bajeti halisi, hutokana na makusanyo ya kodi.

Baada ya migomo hiyo iliyotikisa katika mikoa mbalimbali, serikali ilikubali kukutana na wafanyabiashara hao, wakiwakilishwa na wenzao wa Kariakoo ambao walitoa madukuduku yao mbele ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, ambaye aliahidi kuyafanyia kazi. Mkutano huo wa wafanyabiashara na serikali pia ulisababisha mabadiliko ndani ya TRA ambayo yalimgusa mtendaji mkuu wa mamlaka hiyo.

Nuru ya kuweka mazingira bora kwa wafanyabiashara na kuondoa kero zao imeanza kuonekana baada ya juzi, TRA kutangaza kuanza kutatua migogoro ya wafanyabiashara kwa kuweka utaratibu wa kukutana nao mara tatu kwa mwezi ili kuwasikiliza.

Kamishna Mkuu wa TRA, Yussuph Mwenda, wakati akizindua APP (application) ya TRA Sikika', kwa ajili ya kupokea maoni, ushauri na malalamiko kutoka kwa wafanyabiashara na wananchi ambayo yatamfikia Kamishana Mkuu moja kwa moja, alisema pamoja na kupokea maoni hayo, atakuwa anakwenda kukutana na wafanyabiashara hao na kufanya mazungumzo ambayo kwa kiasi kikubwa yataondoa kero nyingi zilizopo sasa.

Mwenda alisema wafanyabiashara wa Kariakoo, mathalan, miongoni mwa mambo yaliyojitokeza katika kikao na Waziri Mkuu hivi karibuni ni kuingiza mizigo kutoka nje kwa kuchangia na mtu mmoja kulipia ushuru wa forodha. Katika kutatua hilo, alisema mamlaka imeshatengeneza timu kwa ajili ya kutatua kero hiyo.

Kabla ya kufikia hatua ya kuanza kukutana, Mwenda pia alisema masuala ya makadirio ya ushuru wa forodha yameshaanza kupatiwa ufumbuzi na hivi sasa mfanyabiashara wa vitenge anajua kiwango cha ushuru anapoagiza bidhaa hiyo.

Jambo la kufurahisha ni kwamba Mwenda mpango wa serikali, kama alivyosema Mwenda, ni kuifanya Kariakoo kuwa soko la kimataifa na lenye ushindani katika nchi za kusini mwa Jangwa la Sahara huku akiweka bayana kwamba haipendezi kuita soko la kimataifa wakati watu wa nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) hawafiki na kununua bidhaa.


Ni wazi kwamba TRA imedhamiria kwa dhati kuhakikisha kunakuwapo mazingira wezeshi kwa wafanyabiashara kufanya shughuli zao, hivyo kuiwezesha serikali kupata mapato stahiki.

Hatua ya kuweka utaratibu wa kukutana na wafanyuabishara ni mwafaka na umo katika 4R za uongozi wa Samia ambao unataka kuwe na maridhiano baina ya pande husika.

Kwa hiyo kukaa na wafanyabiashara na kuzungumza ni hatua itakayowezesha pande husika (TRA na wafanyabiashara) kuzungumza na hatimaye kufikia mwafaka utakaowezesha kuongezeka kwa mapato ya serikali.

Wahenga wanasema utamkamuaje ng'ombe maziwa ilhali humpi mashudu? Ndivyo ilivyo kwa wafanyabiashara wanavyotakiwa kuwekewa mazingira bora ya ufanyaji shughuli zao ili kulipa kodi halali na stahiki kwa maendeleo ya taifa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Hii ni fursa kwa kila Mtanzania mwenye sifa kujiandikisha

Na Sabato Kasika

**TUME** Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC) iko mikoani ikiendelea na kazi ya kuboresha daftari la kudumu la wapigakura.

Wakati kazi hiyo ikiendelea, ni vyema pia kuwakumbusha Watanzania umuhimu wa kujiandikisha kwenye daftari hilo kwa sababu wako baadhi ya watu ambao huwa wanasema: "Siasa tuwaachie wanasiasa tutafute pesa kujikwamua kimaisha, hatima ya maisha yetu iko mikononi mwetu" wanasahau kuwa siasa ni maisha, hivyo si rahisi kuikwepa.

Siasa haikwepeki kwani viongozi kuanzia ngazi ya kitongoji, kijiji, mtaa, kata, majimbo na taifa, wanatokana na siasa, na ndio wanaoamua mambo mbalimbali yanayohusu maendeleo na maisha ya jamii kwa ujumla.

Ukweli ni kwamba siasa ndiyo ambayo huathiri bei za bidhaa mbalimbali na suala la kupanda au kushuka kwa kodi, kwa sababu wahusika wakuu kwenye maamuzi ni wale ambao wanatokana na siasa.

Wanatokana na siasa kwa sababu wanachaguliwa kupitia sanduku la kura, hivyo ni muhimu kila mwenye sifa za kupiga kura akajihusisha na siasa, kwa maana ya kuchagua viongozi sahihi kwa ajili ya maendeleo.

Kama watu wataendelea kujitenga na siasa, wakidhani haiwahusu, inawezekana wakawa wanachangia kupatikana viongozi ambao si sahihi, watakaokwamisha maendeleo, kwa kukosa sifa na uwezo wa kuongoza.

Ni vyema kila Mtanzania mwenye sifa kushiriki kwenye uchaguzi, ajihusishe, kwani Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inaboresha daftari la kudumu la wapigakura, ili kumpa fursa kila mwenye sifa. Daftari linaboreshwa ili kila aliyefikisha umri wa miaka 18 aandikishwe na hatimaye ashiriki katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2025 kupata viongozi watakaoongoza nchi kwa miaka mitano ijayo.

Julai 20, mwaka huu, kazi ya uboreshaji wa daftari hilo, ilianzia katika mkoa wa Kigoma kwa muda wa siku saba, kisha mikoa mingine huku tume ikitumia muda wa siku saba kwa kila mkoa.

Ikumbukwe kuwa, kila mara tume imekuwa ikihimiza watu kujiandaa kujiandikisha au kuboresha taarifa zao, kwani inajua umuhimu wa Mtanzania aliyetimiza umri wa miaka 18 kushiriki uchaguzi huo.

Ni kwa sababu inatambua kuwa siasa ni njia ya kufanya maamuzi katika ngazi mbalimbali, kwani katika demokrasia, kila mtu ana kiasi fulani cha nguvu, kwa hiyo siasa ya demokrasia watu wote huchangia uamuzi.

Ninadhani si sahihi kutojiingiza katika siasa halafu watu wengine wanapochagua viongozi ambao labda hawawezi kuongoza, wanaanza kulaumu wanasiasa na kumbe wao ndio wamechangia hali hiyo. Kushiriki katika uchaguzi kwa kuchagua viongozi ni jambo sahihi, lakini kujiweka pembeni, kwa maelezo kuwa hawataki kujiingiza katika siasa, kunaweza kuchangia kupata viongozi wasiofaa.

Ingefaa kila mmoja kutafakari na kisha kuchukua hatua za kushiriki katika uchaguzi, kwa kujiandikisha katika daftari la kudumu la wapigakura au kuboresha taarifa kwa wakati.

Ingekuwa vyema wakati daftari halijafika mkoani kwetu, tujipange kufika kwenye vituo vya kujiandikisha ili kutoa taarifa sahihi na kupata kadi na kujiandaa kushiriki kwenye uchaguzi ujao.

Lakini pia wakati tume inaendelea kuboresha daftari hilo, ni vyema kukumbuka kuwa mwaka huu kuna uchaguzi wa viongozi wa vitongoji, vijiji na mitaa, wenye kadi za kupigia kura wasijiweke pembeni.

Hii ni kwa sababu wapo baadhi ya watu ambao wamekata tamaa baada ya kupigia kura wagombea wao, lakini baada ya matokeo kutangazwa, wakawa wameshindwa. Baadhi yao husema hawataki kushiriki uchaguzi kwa madai kwamba hata wakipiga kura, watachaguliwa wengine, hivyo wanaona ni bora waachane na masuala ya siasa au uchaguzi.

Ikumbukwe kuwa wanaojiweka pembeni, na kubaki wakilalamika, wataendelea kusababisha wachaguliwe wale ambao si chaguo lao. Hivyo, njia nzuri ni kushiriki uchaguzi bila kuchoka hadi kieleweke.

Tusikwepe siasa, tujiandae kujiandikisha na kuboresha taarifa zetu, lakini pia tukumbuke kuwa uchaguzi wa viongozi wa serikali za mitaa uko mlangoni, tujipange kuchagua viongozi sahihi.

# MAKALA

**FIKRA MBADALA**

## Ni aibu kuagiza chakula, mafuta ya kupikia ughaibuni



Pascal Mayalla

TANZANIA ni nchi inayotegemea kilimo. Uchumi wa Tanzania unategemea kilimo na asilimia 80 ya Watanzania wanategemea sekta hiyo. Ndiyo maana kumekuwa na msemo kwamba kilimo ndio uti wa mgongo wa taifa. Hii ni kwa sababu sekta ya kilimo (mifugo na uvuvi vikiwamo) ndiyo tegemeo kubwa la viwanda mbalimbali.

Pamoja na hayo, ukweli ni kwamba makundi ya wakulima, wafugaji na wavuvi ndiyo yanayoishi kwenye umaskini uliotopea. Kama nchi yetu inategemea kilimo, kwa nini wakulima ni masikini wa kutupwa na wanaishi kwa kipato cha chini ya dola moja kwa siku?

Tangu tumepata uhuru mwaka 1961, Mwasisi wa Taifa la Tanganyika na baadaye Tanzania, Mwalimu Julius Nyerere, alitangaza kuwa tunao maadui watatu ambao ni ujinga, maradhi na umaskini

Hata leo, ikiwa ni zaidi ya miaka 60 ya uhuru, maadui hao hao bado tunao na pengine wameongezeka wawili, yaani rushwa na ufisadi.

Tanganyika (kabla ya kuungana na Zanzibar mwaka 1964 na kuanzishwa taifa la Tanzania) ilipata uhuru wakati mmoja na nchi zinazojulikana kama Asian Tigers - Korea Kusini, Taiwan, Indonesia, Singapore na Malaysia na hali ya pato ghafi la taifa (GDP) lilikuwa linafanana na nchi hizo. Lakini sasa ukifika kwenye nchi hizo ukaambiwa tulipata nazo uhuru, tena zikiwa hazina chochote kulinganisha na rasilimali tulizo nazo, hakika utashangaa. Kwa sasa tulipo sisi na wenzetu walipo , kama una machozi ya karibu, unaweza kulia.

Ukilinganisha na mataifa hayo, Tanzania imejaliwa kuwa na kila kitu cha kuiwezesha kupiga hatua kubwa kimaendeleo. Kusema ukweli nchi hizo hazina hata nusu ya rasilimali zilizopo Tanzania.

Tanzania imejaaliwa ardhi kubwa ya kutosha ya udongo wenye rutuba kuotesha kila zao tunalohitaji kwa chakula na biashara kutosheleza mahitaji ya ndani na hata ziada kuuza nje. Tumejaaliwa vyanzo vingi vya maji vya kuendesha 'schemes' za kilimo cha umwagiliaji. Kwa mantiki hiyo, mazao ya chakula kama mpunga, mahindi, maharage na vile vya mizizi kama viazi, mihogo na maghimbi zinaweza kuzalishwa kwa wingi na wanaojihusisha na kilimo cha mazao hayo kuwa matajiri wa kiwango kikubwa.

Kadhalika mazao ya biashara kama chai, kahawa, pamba, katani, pareto, miwa kwa ajili ya uzalishaji wa sukari, karanga, alizeti na michikichiki kwa ajili ya mafuta ya kupikia na ngano kwa matumizi ya nyumbani na viwandani yanaweza kuzalishwa kwa wingi na viwanda vikapata malighafi za kutosha na zingine kuuzwa nje.

Kwa mantiki hiyo, Tanzania ilipaswa kuwa nchi ya kuuza zaidi bidhaa zake nje kuliko ilivyo hivi sasa! Kwa kweli, kwa hali ilivyo sasa, ni aibu kwa Tanzania kuagiza chakula, mchele, unga wa ngano, sukari na mafuta ya kupikia.

Enzi za Nyerere, tulifuata mfumo wa siasa ya Ujamaa na Kujitegemea, tukitumia kaulimbiu ya "ili tuendelee tunahitaji watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora (kwa sasa tunaweza kusema utawala bora)". Pia tuliamini kwamba fedha si msingi bali ni matokeo. Vitu hivyo vinne vilikuwapo enzi za Nyerere na bado vipo. Swali ni kwani hatuendelei?

Zilianzishwa programu mbalimbali za kilimo kwa kuanza na operesheni vijiji, ikaja siasa ni kilimo, kilimo cha kufa na kupona. Wananchi walilima kwa juhudi kubwa na hata kujitosheleza kwa kilimo cha chakula kama vile mahindi na ngano. Kama tuna kila kitu cha kutufanya tuendelee, kwa nini Tanzania bado ni maskini? Tulifanya kosa moja kubwa kusema fedha sio msingi wa maendeleo, fedha ni matokeo, ukweli ni kwamba fedha ndiyo kila kitu. Nasema hivyo kwa sababu fedha ndio mtaji mkubwa kwa ajili ya kuliwezesha taifa kufanya mambo mbalimbali hasa kutokana na mabadiliko ya sasa ya sayansi na teknolojia.

Wakati Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere, anangatuka katika uongozi mwaka 1985, alikubali makosa na kusema: "Kufanya kosa si kosa bali kosa kurudia kosa." Japo Mwalimu Nyerere hakusema kosa lenyewe ni nini, ukweli ni kwamba kubwa Tanzania jambo lililolifanya hadi kusababisha mamilioni ya watu kuishi kwenye umaskini uliotopea, ni kudharau fedha na uwekezaji kwenye kilimo.

Kilimo cha jembe la mkono ni cha kujikimu tu, hivyo hakiwezi kumkomboa mkulima kutoka katika lindi la umasikini sambamba na kilimo cha kutegemea mvua. Suluhisho la ukombozi wa kilimo ni kilimo biashara cha kutumia zana bora na za kisasa za kilimo zinazokwenda sambamba na mabadiliko ya sayansi na teknolojia.

Wakati wa Maonesho ya Kimataifa ya Wakulima, maarufu kama Nanenani yaliyofanyika katika kanda mbalimbali nchini lakini kitaifa yakaadhimishwa kwenye Nzuguni, Dodoma, nilishuhudia mamia ya zana bora na za kisasa za kilimo zikiongozwa na kampuni ya Agricom Africa ambayo si tu imemwaga matrekta ya kutosha, bali pia inajenga kiwanda cha kuunganisha zana hizo kwa ushirikiano na kampuni ya Mahendra ya India. Huu sasa ndio ukombozi wa kweli kwa sekta ya kilimo.

Rais Dk. Samia Suluhu Hassan wakati wa kilele cha maonesho hayo, alisema Serikali imejipanga kujenga uchumi jumuishi unaowainua wananchi wote na kuwawezesha kunufaika ipasavyo kupitia uwekezaji unaofanywa katika sekta za kilimo, mifugo na uvuvi.

Katika kufikia njozi hiyo, Rais Samia alisema serikali imeongeza bajeti kwa ajili ya kilimo, mifugo na uvuvi ili uwekezaji huo ulete mageuzi makubwa kwa kuongeza maeneo ya umwagiliaji, matumizi ya mbolea, uzalishaji na usambazaji wa mbegu bora, kuimarisha huduma za ugani, kuboresha miundombinu ya kuhudumia mifugo na upatikanaji wa huduma za ugani, chanjo, majosho na masoko.

Rais Samia pia alisema serikali imeendelea na ujenzi na ukarabati wa viwanda vya uchakataji wa mazao ya mifugo, ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya uvuvi, ukuzaji wa viumbe maji na utafutaji wa masoko na utoaji wa mikopo yenye masharti nafuu kwa wavuvi na wafugaji.

Pia alisema lengo la kujenga uchumi jumuishi ni kuongeza tija katika sekta za uzalishaji na kupunguza umaskini wa kipato kwa mwananchi mmoja mmoja na kutumia sekta za kilimo, mifugo na uvuvi kutengeneza ajira. Jitihada hizi, alisema zina lengo la kusaidia Tanzania kuhakikisha upatikanaji wa chakula na kuhakikisha zina mchango katika pato la taifa na uchumi kwa ujumla.

Rais alisisitiza kwamba serikali inalenga kuongeza bajeti katika utafiti ndiyo maana maabara na vituo vya utafiti vimezinduliwa ili kuwezesha nchi kufikia masoko ya kimataifa kupitia utafiti.

**Paskali**
**+255 754 270403**

## WMA yapongeza wakulima Karatu kuzingatia matumizi sahihi vipimo

**Na Veronica Simba,** KARATU

KAIMU Mkurugenzi wa Huduma za Ufundi wa Wakala wa Vipimo Tanzania (WMA), Albogast Kajungu, amefanya ziara ya kushtukiza katika mashamba ya vitunguu eneo la Mang'ola, Karatu mkoani Arusha na kuridhishwa na wakulima wanavyozingatia matumizi ya vipimo sahihi.

Akizungumza na timu ya wataalamu wa WMA juzi wakati wa ziara hiyo , Kajungu alisema lengo ni kujiridhisha ikiwa wananchi wanazingatia elimu inayotolewa na wakala kuhusu matumizi ya vipimo sahihi ili kulinda pande zote, yaani wakulima, wafanyabiashara na watumiaji wa bidhaa.

Katika ziara hiyo, timu hiyo ya wataalamu wa WMA, walihakiki uzito wa vitunguu vilivyofungashwa katika vifungashio vya aina mbalimbali tayari kuuzwa pamoja na kuzungumza na wakulima, wafanyabiashara na wasafirishaji wa mazao hayo.

"Niwapongeze sana kwa kuzingatia matumizi ya vipimo sahihi maana katika mazao yote yaliyofungashwa ambayo tumepima, hakuna yaliyozidi uzito unaoelekezwa kisheria. Nawasihi mwendelee hivyo kwani kila upande utapata faida stahiki," alisema Kajungu.

Kuhusu maelekezo ya kisheria kwa uzito wa mazao ya shamba yaliyofungashwa, Kajungu alisema mkulima yuko huru kufungasha kwa kutumia aina yoyote ya kifungashio isipokuwa azingatie uzito usizidi kilo 100.

Alitoa ufafanuzi huo kutokana na uelewa tofauti kwa baadhi ya watu wanaotafsiri kuwa sheria inakataza kufungasha mazao kwa kuongeza kishungi katika vifungashio.

"Niendelee kuwaelimisha na kuwaelewesha kuwa tafsiri sahihi ya lumbesa si kishungi bali ni uzito uliozidi kilo 100 kwa mazao yaliyofungashwa. Katika hili niseme wazi huwezi kuthibitisha lumbesa kwa macho, hivyo ni lazima upime kujiridhisha kuwa mazao yaliyofungashwa yamezidi kilo 100," alisisitiza.



Kaimu Mkurugenzi wa Huduma za Ufundi kutoka Wakala wa Vipimo (WMA), Albogast Kajungu (kulia), akiongoza uhakiki wa uzito wa vitunguu vilivyofungashwa tayari kwa kuuzwa katika eneo la Mang'ola, Karatu, mkoani Arusha jana. **PICHA: WMA**

Katika hatua nyingine, alishauri halmashauri zote nchini kutumia mizani kupima mazao yaliyofungashwa ili kuondoa utata na manung'uniko yanayojitokeza kwa baadhi ya wakulima na wafanyabiashara kwamba wanatozwa faini kwa mazao yaliyofungashwa na kuwa na kishungi yakitafsiriwa kama lumbesa.

"Mwarobaini wa changamoto hiyo ni kutumia mizani kama sheria inavyoelekeza na si kutizama kwa macho," alisema.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, wakulima na wafanyabiashara wa vitunguu katika eneo la Mang'ola walikiri kunufaika zaidi kila upande baada ya kuanza kuzingatia elimu ya vipimo sahihi waliyopatiwa na serikali kupitia WMA.

Marietha Tlemai, mmoja mkulima wa vitunguu, alipongeza serikali kupitia WMA kwa kuwajali wakulima na kuweka sheria ya ufungashaji mazao inayolenga kulinda maslahi yao.

Awali, timu hiyo ya wataalamu kutoka WMA, ilitembelea ofisi ya mkuu wa wilaya ya Karatu ili kueleza dhamira ya ziara yao na kupokewa na Katibu Tawala, Dk. Lameck Karanga, ambaye aliwahakikishia kuwa ofisi yake inaunga mkono jitihada za kutokomeza lumbesa ili kulinda maslahi ya wananchi ambao wengi hujishughulisha na kilimo cha vitunguu.

AGNESS KAHAMBA

# Mwanadada Mtanzania anayeng'ara kimataifa

## -Ni kutokana na utetezi wa wanawake na watoto

Na Mwandishi Wetu

CHANDA chema huvikwa pete." Ni msemo uliozoeleka ukimaanisha kwamba kitu chochote kilicho chema hupewa tuzo. Kwa maneno mengine, mtenda mema hulipwa mema.

Hivi ndivyo inavyosadifu kwa mambo anayoyafanya Agness Kahamba, binti wa Kitanzania aliyejipatia umaarufu duniani na kupata tuzo kadhaa kutokana na mambo makubwa aliyoyafanya ndani ya muda mfupi katika kutetea haki za wanawake, vijana na watoto.

Tangu mwaka 2018, Agness ambaye ni Mwasisi na Rais wa Tupaze Sauti Foundation (TSF), taasisi isiyo ya kiserikali (NGO) na Balozi wa Kutetea Unyanyasaji dhidi ya Watoto, ameshatwaa tuzo kadhaa ambazo zimemfanya kuwa miongoni mwa Watanzania waliopata umaarufu katika medani ya kimataifa.

Hivi karibuni, Agness alipata Tuzo ya Wanawake Maarufu Afrika 2024 (Most Notable Women in Afrika 2024) katika masuala ya familia na maendeleo ya jamii. Tuzo hii imemfanya kuwa mmoja wa watu 100 mashuhuri barani Afrika.

Tuzo hii imekuja baada ya mwaka jana kupata tuzo ya mmoja ya watu 100 wa juu waanzilishi wa NGO. Alipata tuzo hiyo kwa kutetea na kuleta mabadiliko katika maisha ya watu kwenye masuala ya usawa wa jinsia, ukatili dhidi ya watoto, elimu, afya, uwezeshaji wanawake, haki za binadamu na maendeleo ya jamii. Tuzo hizo zilikuwa mwendelezo wa ile aliyoipata mwaka 2018 baada ya kushika nafasi ya 16 ya Tuzo ya Vijana 50 wa Tanzania wenye Ushawishi.

Mambo hayo hayakupatikana kwa urahisi bali kwa kazi kubwa na yenye kujituma katika yale aliyothubutu kuyafanya baada ya kuanzisha TPF mwaka 2008 kwa lengo la kupinga unyanyasaji wa kijinsia, ukatili dhidi ya wanawake na watoto na uwezeshaji kwa vijana.

"Malengo ya asasi yetu ni pamoja na elimu kwa jamii, kuwawezesha vijana kujitambua, ujasiriamali kwa wanawake na kutambua haki zao. Pia uhamasishaji katika kukabilinana na matukio ya dharura yakiwamo magonjwa ya mlipuko kama ilivyokuwa UVIKO- 19," alibainisha katika mahojiano maalum na Nipashe Jumapili.

"Mimi ni mwanamke, mama, binti na kijana, hivyo niliona hayo maeneo ni ya muhimu kuyafanyia kazi kwa sababu yananihusu kwa namna tofauti. Makundi haya ndiyo yenye shida katika jamii. Kwa serikali pekee ni vigumu kutatua shida za makundi hayo bila msaada wa wadau. Kwa hiyo niliona ni fursa kuanzisha asasi hii kuwezesha jamii kupaza sauti hatimaye serikali ipate taarifa kuzipatia ufumbuzi changamoto hizo kwa haraka," anasisitiza.






Agness Kahamba akiwa na Mhariri Mtendaji wa Nipashe, Beatrice Bandawe. Pichani juu, akiwa ameshika tuzo aliyoipata hivi karibuni ya mmoja wa Wanawake Mashuhuri Afrika. **PICHA: JOHN BADI**

**TUZO CHACHU**

Kuhusu tuzo hizo, Agness alisema zimekuwa kichocheo kwake katika kusonga mbele kwenye malengo aliyojiwekea kupitia asasi ya Tupaze Sauti.

"Tuzo hizi zimeniweka katika viwango vikubwa na kunifanya niendelee kufanya mambo makubwa katika jamii. Hii (tuzo) ya sasa ndiyo imenitambulisha kwa mchango wangu na kuwa miongoni mwa wanawake wanaojitoa kupigania haki za makundi maalum hasa wanawake, vijana na watoto.

"Siku nilipopokea email (baruapepe) kuwa nimepata tuzo hii kutokana na kazi walizoziona kwenye mitandao yangu ya kijamii hasa Linkedin, hususan kutetea vijana na watoto na maendeleo ya jamii, nilipata furaha sana lakini kubwa ilinichochea zaidi kuendelea kufanya majukumu yangu kwa viwango vya juu," alisema.

Pia alisema tuzo hizo zimedhihirisha namna alivyojitoa katika kuwatetea watu wa makundi hayo maalum ambayo yamekuwa yakipitia changamoto mbalimbali.

Kwa mujibu wa Agness, wanawake kwa mfano, kwa miaka mingi wamekumbana na vitendo vya unyanyasaji hasa vipigo kutoka kwa waume zao na wengine kupata ulemavu wa kudumu.

Kutokana na hali hiyo, alisema TSF iliona ni vyema kujitosa na kuwatetea ili wajue haki zao na hatimaye kujikomboa dhidi ya ukatili na unyanyasaji huo.

"Katika hili, tunatoa elimu kwa wanawake ili kutambua haki zao. Katika baadhi ya maeneo, mfumo dume umekithiri. Wanawake wanakandamizwa na hata kukosa haki zao za msingi licha ya kwamba unapungua kutokana na elimu na uhamasishaji unaofanywa na wadau mbalimbali," alisema.

Agness alibainisha kwamba wanawake katika baadhi ya maeneo, hasa vijijini ambako mwamko wa elimu kwa mtoto wa kike ulichelewa, kumekuwa na dhana iliyojengeka kutokana na imani kwamba mwanamke anapoolewa hawezi kuachana na mume hadi kifo kitakapowatenganisha.

Hali hiyo, anasema imewafanya baadhi ya wanawake kuamini kuwa ni mwiko au dhambi kuachana na mume baada ya kufunga ndoa. Alisema kutokana na fikra hiyo, baadhi wanaogopa aibu ya kuonekana kuwa wameondoka kwa waume zao, hivyo wanalazimika kuvumilia hata wakipata vipigo, ulemavu wa kudumu hata kupoteza viungo.

"Kwa kweli katika hili la utetezi na elimu kwa wanawake dhidi ya ukatili na unyanyasaji wa kijinsia, kwa kushirikiana na wadau wengine, tumefanikiwa kwa kiasi kikubwa. Wanawake hivi sasa kwa sehemu kubwa wanatambua haki zao na kujikita katika uzalishaji na kumiliki mali," alisema.

Licha ya wanawake, haki za mtoto hasa wa kike, alisema limekuwa la kipaumbele ili kuwawezesha watoto wa kike kupata elimu na kuwaepusha na ndoa za utotoni, ukeketaji na unyago.

Kwa vijana, alisema lengo kubwa ni kuwafanya wajitambue na kupata maarifa ya kufanya kazi badala ya kuwa na fikra kwamba maendeleo yatapatikana kwa njia ya mkato au kufanya michezo ya kubashiri (betting).

"Baadhi ya vijana wamekuwa wakidanganyana kuwa illi kuwa na maisha mazuri lazima uende nje. Wengine wamwekuwa wakijiingiza katika vitendo vichafu kama ushoga ambavyo ni hatarishi kwa afya na maisha yao. Kupitia programu mbalimbali, TSF tunawaelimisha kuhusu stadi za kazi na maisha na kujitambua kuhusu maisha yao kwa ujumla," alisisitiza.

**MAFANIKIO**

Tangu kuanza kwa TSF, Agness alisema kumekuwa na mafanikio makubwa. Moja ya mafanikio hayo ni mapambano dhidi ya ukeketaji, ndoa za utotoni na unyago.

Kwa mujibu wa Agness, utekelezaji wa programu za asasi hiyo zilizofanyika katika mikoa minane nchini, umesaidia kupunguza ukatili dhidi ya wanawake na watoto na kupata elimu kuhusu haki zao. Pia alisema vijana wengi wamejitambua kuhusu maisha yao na mustakabali wao.

"Katika Wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma, vitendo vya unyago kwa watoto wa kike vilikithiri pamoja na ndoa za utotoni. Wazazi walikuwa chanzo cha kushamiri kwa vitendo hivyo kwa tamaa ya kupata mahari wanapowaozesha na pia mila na desturi zao. Tulifanya kila juhudi na sasa hali ni tofauti na ilivyokuwa awali. Vitendo hivyo vimepungua kwa kiasi kikubwa.

"Tulifanya kampeni ya kutokomeza vitendo hivyo kwa kutembelea shule nane kutoa elimu kuhusu umuhimu wa elimu badala ya ndoa. Tulitoa elimu kwa wazazi kuhusu madhara ya unyago na ukeketaji kwa sababu wazazi walikuwa mstari wa mbele kwa ndoa za utotoni kutokana na tamaa ya fedha kwa kutoza mahari na wakati huo huo wanakatisha ndoto za mabinti za kuwa watu mashuhuri baada ya kupata elimu.

"Katika kampeni ile, tuliongozana na mkuu wa wilaya na ofisa elimu wa wilaya kutoa elimu kuhusu madhara ya ukeketaji, unyago na ndoa za utotoni. Pia polisi walikuwapo na waliwaambia waziwazi wazazi kuwa yeyote atakayeendelea na vitendo hivyo atachukuliwa hatua. Kwa kweli hili lilileta matokeo chanya," alisema.

Licha ya kufanikiwa huko, alisema kwa wale watoto wa kike waliokeketwa, walikuwa wakipelekwa kupimwa afya kwa sababu walikuwa wakifanyiwa vitwendo hiyo kwa wembe au kisu kimoja, hali ambayo ni hatari kwa afya zao.

Aidha, Agness alisema baada ya kufanya kampeni hiyo, walirudi walayani humo kwa ajili ya ufuatiliaji na kutoa msaada kwa waathirika na kubaini kwamba kuna mabadiliko makubwa. Watoto wengi waliokuwa wameolewa, wamerejeshwa shuleni kuendelea na masomo na wengine kupelekwa vyuo vya ufundi.

**BADO CHANGAMOTO**

Pamoja na mafanikio ya asasi yake na wadau wengine katika mapambano dhidi ya ukatili na unyanyasaji, dhidi ya wanawake na Watoto pamoja na vijana kujiingiza katika makundi maovu, Agness alisema bado kuna changamoto kutokana na sababu mbalimbali, likiwamo suala la haki za binadamu.

"Masuala kama haki za binadamu yamesababisha kuwapo kwa vikwazo katika kufanikisha mapambano dhidi ya mambo kama ya ushoga, ndoa za jinsia moja. Hapa hatua zaidi zinapaswa kuchukuliwa ikiwamo kutungwa kwa sheria," alishauri.

# MAISHA

AGOSTI 11, 2024

Nipashe


Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*




Nyama ya ng'ombe na njegere

Ukurasa 14






# MWONEKANO MPYAA

Ukurasa 13

# WATOTO

## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA










| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| S | | P | E | M | B | A |
| I | | | | B | | T |
| N | | B | E | E | | W |
| G | O | A | | Y | A | I |
| I | | N | O | A | | S |
| D | | D | | | | H |
| A | T | O | K | E | | E |


## FUMBO TOTO




Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:

ZNZ, NOA, IPI, WAO, AMANI, CHAMA, ZONGA, ANZIA, UTAWALA, ANZISHA

## TOA TOFAUTI 5




## PAKA RANGI




## AMSHA AKILI

MSAIDIE PAKA APATE NJIA YA KWENDA KUMKAMATA PANYA






Alichokifanya daktari

TOFAUTI ya wazazi wa hapa nchini mtoto wa Tanzania na sehemu zingine wakati anapolala inakuwa kama hivi.

Marekani mtoto anapokwenda kulala huagwa na wazazi wake "usiku mwema mwanangu"

Uingereza wazazi wanamuaga mtoto wao "Pata njozi njema mwanetu"

Hispania anapokwenda kulala wazazi humuaambia "usiku mwema mpendwa wetu"

Tanzania mtoto anapotaka kulala wazazi utawasikia "Kesho uamke mapema, hatutaki kusikia umechelewa na hela ya mihogo utaikuta mezani"

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Kwa nini majaribu ni sehemu ya maisha yako?

KARIBU tena msomaji wangu tuendelee kujadili yaliyomo kwenye mfumo wa maisha yetu ya kila siku. Leo nizungumzie majaribu yanayowapata wanadamu hadi kuwatia kizunguzungu wasijue nini hasa kinachosababisha yatokee kwenye maisha yao.

Katika jaribu mtu ana uhuru wa kuchagua kuwa mwaminifu au kutokuwa mwaminifu kwa Mungu. Lakini pia Mungu huwa anaturuhusu kupitia jaribu ili imani yetu ikue.

Majaribu yanaweza kuwa na manufaa kwetu ingawa yanaonekana kutusababishia maumivu. Ni muhimu kwa sababu yanaweza kutufanya pia tuwe wanyenyekevu na kutufundisha kusimama katika imani.

Watu wengi wamekuwa na imani haba kiasi cha kufikia hatua kumkufuru Mungu wasijue kwamba majaribu ni sehemu ya maisha ili kuimarika zaidi kiimani. Ndiyo maana nimekuwa nawashauri watu kwamba unapopata tatizo, usikurupuke kumtukana Mungu au kuanza kumlalamikia na kumnung'unikia.

Yako mambo mengine Mungu huruhusu yatokee kwenye maisha yetu ili tu amdhihirishe yule mwovu kuwa wewe unampenda Yeye (Mungu) kama Baba na muweza wa mambo yote.

Unapoona wewe unamtumikia Mungu, unamcha Mungu, unaishi maisha ya kupendeza na hata unaruhusu sehemu ya mali zako zimtumikie Mungu, lakini ukashangaa kuona unapata pigo kubwa kwenye maisha yako, tambua kuwa kiko kitu Mungu anataka kumthibitishia Shetani.

Kwa hiyo simama hadi mwisho na mtetee Mungu katika mazingira hayo; na Mungu atajitwalia utukufu kupitia wewe. Kumbuka shetani ni mshitaki wa mwanadamu tangu zamani; siku zote anamuonea wivu mwanadamu na anatamani wanadamu wote watupwe chini kama yeye alivyotupwa chini.

Katika jamii yetu, familia zetu nyingi zinapitia magumu mengi kimaisha. Yapo matatizo kama ya elimu, ndoa, matatizo kwenye taaluma na kazi, afya, kufiwa na watu wako wa karibu uliowapenda na matatizo ya uchumi.

Ziko familia ambazo shetani amepata nafasi kuzishambulia na kusababisha maumivu yasiyoelezeka. Kama wewe msomaji wangu ni mmoja wa waathirika wa majaribu ya shetani, hupaswi kukata tamaa wala kumkufuru Mungu.

Mara nyingi baadhi ya watu wana tabia ya kumwabudu, kumsifu, kumtumikia Mungu na kumshukuru tu wakati wanapopata mema. Ikitokea wamepatwa jambo baya, basi hukurupuka kumtupia lawama na kuanza kumtukana na kumdhihaki Mungu.

Jiulize, je, ni mara ngapi umemshukuru Mungu katika mazingira magumu uliyokuwa unapitia? Angalizo; yapo matatizo au majaribu ambayo Mungu huruhusu yatokee ili kupima upendo na uaminifu wetu kwake. Ukiyashinda anakupeleka kwenye utukufu mwingine!

Ziko aina za majaribu. Yale yatokanayo na kujisababishia mwenyewe. Yako mambo mengine mabaya ukiyafanya iwe kwa kujua au kutokujua yanaweza kukupitisha mahali pagumu. Na kama hutaomba rehema na huruma za Mungu yanaweza kukuangamiza kabisa.

Mungu mwenyewe ameshaweka wazi kwamba, tusidanganyike kwani yeye hadhihakiwi kwa kuwa chochote apandacho mtu ndicho atakachovuna (Wagalatia 6:7).

Matatizo mengine yanaweza kusababishwa na chanzo (chimbuko lako), misingi yako, wazazi wako, ndugu zako, mume au mke wako, watoto wako na hata marafiki zako.

Matatizo haya yanaweza kusababisha maumivu makali na kama hutakuwa makini kuyashughulikia yanaweza kukuangamiza. Hivyo ni vema kutafuta ufumbuzi wa kudumu kabla hayajakuangamiza!

Pia yako matatizo/majaribu yanayoletwa na shetani na mawakala zake. Majaribu ya shetani yanakuwa na lengo la kukuangamiza wewe na uzao wako wote na mali zako.

Majaribu ya shetani na mawakala zake kama hayajapata ufumbuzi wa kudumu wa kiroho yana madhara makubwa hivyo usipuuze. Majaribu ya aina hii yanapokuja unapaswa kufanya juu chini kuhakikisha unamwaibisha shetani na mawakala wake kwa kuyageuza matatizo kuwa shuhuda.

Wengi wamekutana na majaribu hawakuvumilia. Wakashindwa kuelewa kuwa hakuna jaribu lisilo na mlango wa kutokea. Lazima utulie ujitafakari jaribu hilo linatokana na nini?

Nimeeleza mara nyingi kwamba hakuna kitu kinachotokea kwa bahati mbaya pasipo kuwa na chanzo. Nimeeleza hapo juu kwamba majaribu mengine yanatokana na kujisababishia, yaweza kuwa ni misingi mibovu ya chimbuko lako, wazazi wako na kadhalika.

Na kwa sababu shetani ni mshitaki wetu, Mungu huruhusu majaribu ili ujitafakari ulipoanguka. Lipo kosa unaloweza kulifanya, ukalijutia maisha yako yote.

Tena unalifanya pale Mungu anapotaka kukupa muujiza wako. Msomaji wangu, kumbuka kwamba katika kila hali unayopitia, Mungu ana kitu anachokufundisha wewe na watu wanaokuzunguka. Una maoni ujumbe 0715268581.

**Tukutane wiki ijayo.**

## WARAKA WA NDANI
Na Godfrey Mushi



# Waliokuonea wivu, kufurahia mapito yako bado wapo

WENYE hila waliumbwa wengi. Namna siasa za hapa nyumbani zinavyoendeshwa kwa sasa ni kama zimegeuzwa kuwa ajira ya kudumu au biashara ya watu fulani.

Ajabu ya Mussa! Leo mtu yuko chama fulani, kesho anaamka yuko chama kingine chenye misingi tofauti na ile ya chama chake alichoondoka.

Huko makao mapya, anashupaza mishipa ya shingo akieleza tofauti yake ya kimtizamo, wakati aliishi huko na akatuaminisha kwa miaka yote wao ndio wapigania haki wa kweli.

Unataka nikuambie nini tena ili ujue siasa ni biashara? Ngoja, nitafute namna bora ya kuzungumza na nanyi tuelewane.

Kuna nyakati, unaweza kuona kabisa kwamba wenye nguvu si wale ambao huwa wanashinda siku zote bali wenye nguvu ni wale ambao hawakati tamaa wakati wanaposhindwa.

Binadamu wanaweza kukuchoma kisu mgongoni, kisha wakaja mbele kukupa pole.

Watakufundisha kila kitu kwenye maisha lakini si kuishi bila wao.Hawatakufundisha kamwe. Jiongeze!

Waswahili wanasema wema una mwendelezo, ila ubaya una mwisho. Kwamba eti wakishindwa kufanya unachokifanya, watapambana kukuharibia. Hakuna ubishani kwamba, muda hauongopi, wote mtapimwa na muda.

Nimelazimika kuanza na bashrafu hiyo kwa sababu ya maneno mazito aliyonukuliwa Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Bara, Tundu Lissu.

Siku chache zilizopita, katika Mtandao wa Club House, kuliibuka mjadala mzito wa kisiasa kuhusiana na joto au mchakato wa uchaguzi mkuu wa Tanzania wa mwaka 2025.

Katika mjadala huo, Lissu amenukuliwa akisema endapo CHADEMA itaacha misingi yake iliyomfanya ajiunge nayo, basi ataondoka katika chama hicho; kwa kuwa si dhambi na CHADEMA si dini na si mama yake.

Akizungumza kupitia mtandao huo, Lissu amemnukuu Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, aliyewahi kusema CCM (Chama Cha Mapinduzi), si mama yake na ikiacha misingi yake ataiacha.

Ameenda mbali zaidi akisema: "Unataka niseme kwa mazingira yoyote yale, vyovyote itakavyokuwa sitahama CHADEMA? ni mama yangu?

"Nitakuwa sina sababu ya kubaki na hiyo siyo dhambi. Ni chama cha siasa. Vyama vya siasa huja na kuondoka, sisi binadamu tunakuja na kuondoka, kwa hiyo usiniombe nijifunge minyororo ya aina hiyo."

Hakika! Maneno haya ya nguli wa siasa za upinzani na mkosoaji mkubwa wa serikali, yamenisukuma kuandika haya nikiamini na mimi ninalo jicho katika siasa zetu.

Kwa mtazamo wangu, tunahitaji viongozi wa kisiasa na hata wasio wa kisiasa, kujenga nguvu kubwa ya ushawishi na majadiliano na watu walio na mitazamo tofauti.

Kwa mfano, kwa namna mbalimbali, inawezekana na wewe uliwahi au umewahi kuwa miongoni mwa watu ambao waliwalaumu ama kuwalaumu wanaohama vyama, kana kwamba wanatumika kisiasa.

Sijui unanielewa! Labda nikuambie hivi utanielewa vizuri. Pasina shaka, wale waliokukimbia, waliokuonea wivu, kufurahia mapito yako bado wapo.

Jenga mazingira ya kuwafanya rafiki zako, wakusaidie kuona upungufu wako na si kuona mazuri yako.

Hiki ndicho kipindi cha kuonyesha wema wako kwao, kusudi watambue kuwa uongozi ni kuwatumikia wote.

Waliofanya juhudi kusudi ushindwe nao pia hawajapoa. Wanaweza kuanzisha juhudi mpya ili kukukwamisha.

Uzoefu unaonesha kuwa watu wa aina hii hujenga urafiki na watu wanaoonewa na wanaotafuta madaraka.

Lakini mara tu watu wakipata madaraka huanza kuwachukia watu wa aina hii.

Mikakati hupikwa. Wakati unapika mikakati yako kuwa makini sana na watu wanaokuzunguka.

Jifunze kuwa na kifua. Tafuta uwezo binafsi wa kuchuja nani rafiki na nani chawa, hiyo itakusaidia. Siasa ni shughuli ya kimaadili inayohusiana na ujengaji wa jamii yenye usawa.

Na binadamu kwa asili ni mnyama wa kisiasa anayeishi kwenye jamii ya kisiasa, kwa hiyo kila kitu kinachofanyika ni siasa.

Siasa si tu kuwakusanya watu na kuwasomea hotuba, kutangaza na kutekeleza ilani ya chama fulani cha siasa, sera na ahadi;siasa ni maisha yetu ya kila siku.

**• Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa barua pepe: ghandsome79@gmail.com Simu ya mkononi: +255 715 545 490**

# HARUSI









Ni tukio la kukumbukwa kwa mwanasheria Denis baada ya kufunga ndoa na Suzan na kufuatia sherehe ya kuwapongeza iliyofanyika ukumbi wa Grand Entrance jijini Dar es Salaam hivi karibuni. PICHA: MC GaraB

# MITINDO

Na Moshi Lusonzo



## MWONEKANO MPYAA

KUTOKANA na ukuaji wa teknolojia, watu sasa hawahitaji kuvaa nguo zilizotengenezwa kwa pamba pekee kama ilivyokuwa zamani.

Suruali laini zinazotengenezwa kwa teknolojia ya Utra, zimekuwa chaguo bora kwa watu mbalimbali hasa vijana kutokana na ubora, mwonekano na mitindo yake ya kipekee.

Nguo hizi zinafaa kuvaliwa sehemu yoyote na katika majira ya joto.

Pia zimetengenezwa zikiwa na matundu madogo ambayo yanasaidia kuingiza hewa na kukinga uchafu kuganda kwenye nguo.


Kwa wanaume wanaweza kuvaa suruali za aina hii wanapokwenda ofisini au katika michezo mbalimbali.

Kufuatia kuwepo kwa mfumo mzuri wa kupumulia, mtu anapovaa anapata ujasiri, kujiamini na kuwa na mwonekano mzuri zaidi.

## UREMBO

Na Mary Geofrey





# Usiteseke tena na usugu kwenye kiwiko, magoti



MARA nyingi ngozi nyeusi kwenye kisugudi au kiwiko cha mkono ama goti husababishwa na mkusanyiko wa seli zilizokufa kutokana na msuguano sehemu hizo.

Kwa kawaida, sehemu hizi huwa kavu na hazina uwezo wa kutoa mafuta kama sehemu zingine za ngozi na hivyo zinahitaji kutunzwa na kufanywa kuwa safi.

Ukiwa na mazoea ya kuweka kisugudi au kiwiko chako kwenya meza wakati unapofanya kazi ama kukutanisha goti lako wakati unapofua, au shambani, ule msuguano hufanya ngozi yako katika maeneo hayo iwe nyeusi.

Hata hivyo kuna njia mbalimbali rahisi za kuondoa weusi huo ambazo zimekuwa zikitumiwa na kina dada hasa nyumbani ambazo zinafanya kazi.

**Tango**

Kama ilivyo kwa ndimu imethibitishwa kuwa tango lina uwezo mkubwa katika kuifanya ngozi kurudi kwenye asili yake.

Ina uwezo mkubwa wa kuzuia ngozi kuharibika na vitamini A na C ambavyo ni muhimu sana katika kuiboresha ngozi na kuifanya iwe laini tena.

Mchanganyiko wako unaweza kuongeza limao kabla ya kuupaka kwenye goti au kisugudi na maeneo meusi unayotaka yawe meupe.

**Ndimu**

Ndimu ina uwezo mkubwa wa kuzuia ngozi kuharibika na vitamini C ambavyo ni muhimu sana katika kuiboresha ngozi na kuifanya iwe laini tena.

Ndimu imethibitishwa kuwa kiungo muhimu katika kuifanya ngozi kuwa nyeupe.

Ina uwezo mkubwa wa kuzuia ngozi kuharibika na vitamini C ambavyo ni muhimu sana katika kuiboresha ngozi na kuifanya iwe laini tena.

Kwa kutumia pamba, kitambaa safi au tunda lenyewe tu, paka juisi ya ndimu iliyochanganyika na magadi kiasi katika sehemu zenye weusi.

Tulia nayo kwa muda wa saa moja kisha osha sehemu hiyo. Rudia kila siku hadi weusi utakapopotea.

## MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Nyama ya ng'ombe na njegere



MARA nyingi kwenye familia za Watanzania imezoeleka mapishi ya nyama ya rosti unaweka viazi au nyanya chungu na bamia.

Mapishi ya nyama kwa aina ya mchuzi au rosti siyo lazima iwe tu ilivyozoeleka, unaweza kupika rosti au mchuzi wako ukaweka na njegere na ukajinoma.

**Mahitaji**

Nyama ya ng'ombe gramu 300, karoti moja, njegere gramu 150, vipande vya vitunguu maji, tangawizi na vitunguu saumu, chumvi kijiko kimoja, mchuzi wa sosi vijiko viwili, sukari vijiko viwili, siki vijiko viwili, maji ya wanga vijiko vitano.

**Namna ya kupika**

Osha nyama ya ng'ombe, halafu uikate iwe vipande vidogovidogo, ondoa maganda ya karoti halafu uikate iwe vipande vidogovidogo.

Washa moto tia mafuta kwenye sufuria, mpaka yawe na joto la nyuzi 60, tia njegere, kaanga, halafu ziepue.

Washa moto tena, tia vipande vya vitunguu maji, tangawizi na vitunguu saumu kwenye sufuria koroga, tia vipande vya nyama ya ng'ombe, koroga halafu tia vipande vya karoti na koroga tena.

Weka tena sukari, siki, mchuzi wa sosi, chumvi, koroga, mimina maji ya wanga, koroga tia njegere koroga kisha uepue na upakue tayari kwa kuliwa na wali, ugali au tambi.

MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya





# Matokeo ya nyumba nzuri ni uimara wa ukuta

NI ndoto ya kila mtu kumiliki nyumba ya viwango vya juu. Swali la kujiuliza nyumba hiyo ni ya namna gani? Nini kinaifanya nyumba kuwa na biwango vya juu?

Yako mambo mengi yanayotoa majibu kwa ajili ya swali hilo lakini ukuta ni sehemu muhimu na ya kudumu ambayo ndiyo hushikilia ustawi na uimara kwenye nyumba au jengo lolote.

Mara nyingine matokeo ya nyumba nzuri na uimara wake huonekana kwa nje ikiwa imenakishiwa vizuri bila kujua siri ya vitu gani vilivyotumika mpaka kufikia kuonekana katika hali hiyo.

Mtaalam wa ujenzi, Victor Mkalama, anasema ukuta anaozungumzia ni ule ambao hutokana na mchanganyiko wa zege au mawe na kufanyiwa utaalam wa uashi na kusimama kama ukuta ambao baadaye huitwa nyumba.

Anasema jambo la msingi la kufahamu katika kutambua kama unataka kuwa na ukuta wa nyumba bora, imara na wa kudumu ni kuhakikisha unakuwa makini na aina ya malighafi unayotumia ambayo inaendana na mazingira ya eneo husika.

Jambo lingine, anasema la kuzingatia ni mtindo na muundo wa nyumba husika katika kuifanya iwe bora na imara.

"Na katika hili unapaswa kufahamu pia kwamba nyumba unayojenga ni ya mtindo na ya muundo gani na pia kama ni wa kutumia mawe au tofali ili fundi anayejenga akushauri kutoka na mazingira ya eneo lako.

"Ukuta bora, imara na ambao ni wa kudumu unategemea sana na aina ya malighafi," anasema na kuongeza kuwa: " Ikumbukwe kwamba ukuta wa tope, mawe au tofali ubora na uimara wake hutofautiana sana, na ndiyo maana tunashauri sana kupata ushauri kutoka kwa wataalam."

"Kwa hiyo hata katika ufundi katika kujenga nyumba yenye ukuta bora hakuwezi kutokana na ubunifu pekee kutoka kwa fundi, unategemeana sana na hivyo vitu vitatu ambavyo ni malighafi, mazingira ya eneo ambalo nyumba husika inajengwa na muundo wake, halafu ufundi ni wa mwisho," anasisitiza.

Pia anasema katika kazi ya kujenga ukuta wa nyumba au wa jengo lolote ni lazima kuzingatia uzito unaoendana na jengo husika.

"Ukuta usioendana na aina ya jengo unaweza kuleta shida kwenye jengo au nyumba baadaye. Na aina ya kwanza ya ukuta unaobeba uzito wa jengo hujengwa kwa kutumia tofali za kuchoma, mawe au tofali za zege au mchanga.

"Kazi ya ukuta wa aina hii hufanya kazi kubwa ya kuchukua na kusafirisha uzito wa paa au jengo hata kama ni nyumba ya kawaida au ghorofa," anasisitiza.



# Tengeneza bustani ya mboga kuwa maua

Na Restuta James

BILA shaka, msomaji wangu unafahamu umuhimu wa mboga katika lishe hasa kutokana na kuwa na kiasi kikubwa cha viini lishe kama vitamini, madini, chumvi na protini.

Utafiti unaonesha kwamba kila mlo wa siku, mboga zinapaswa kuwa ni asilimia 20 ya chakula chote.

Ili kudhibiti ubora wa chakula hiki muhimu, ni vyema kila nyumba ikawa na utaratibu wa kupanda nyumbani kwa ajili ya chakula na wakati huo huo kama maua.

Hili linawezekana kwa kuwa mboga ni zao linaloweza kuleta matokeo makubwa ndani ya muda mfupi kwenye eneo dogo, hasa kwa wanaolima kwa matumizi binafsi.

Ubunifu umesaidia kuwezesha uanzishaji wa bustani za mboga nyumbani, kwa kupanda kwenye makopo, vyungu, viriba, mifuko ya plastiki, magunia au matairi.

Mtaalamu wa bustani, Joseph Massawe, anasema familia inaweza kupanda mboga ambazo inazihitaji kwa kiasi kikubwa na zinastawi vizuri na kwa urahisi.


"Masalia ya jikoni kama maganda ya nyanya, viazi, ndizi, vitunguu na samadi ni mbolea ya kurutubisha wakati majivu na majani kama ya mwarobaini yanaweza kutumiwa kama dawa ya kufukuza wadudu waharibifu," anasema.


**DONDOO MUHIMU**

- Hakikisha unaihudumia vizuri hasa maji na mbolea
- Tumia eneo dogo ili uweze kumudu.
- Mboga za asili ni nzuri zaidi.
- Itumike teknolojia ya asili
- Inawezesha familia kupata mboga salama na inapendezesha mazingira.
- Gharama za chakula kwa familia hupungua.
- Hupunguza utapiamlo na kuongeza usalama wa chakula.



# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2024
SMS - 0713 447766
JUKWAANI
SAFARI HII LAZIMA MAJI NTAITA "MMA" KUDADADEKI!
EH! BABA MBONA LIME-TUKOMALIA TUMELIKOSEA NINI?
"UKATA"
SISI
!


HUYO MTU HAJADO-NDOKA KWA SABABU YA PRESHA, TATIZO LIPO KWA JIRANI YAKE
DUH! KWELI TATIZO NISHALIONA LILILO-MSABABISHA AKOSE HEWA SAFI.
SINGILENDI CHAF! MAK@#PA NAYO NDO USISEME!!! ALAFU KAWEKA MIKONO JUU!
ALIYESABABI-SHA KAUCHUNA KAMA HAYUPO!
KWA NINI HUJITHAMINI HADI UNAKUJA KUSABABISHA MAAFA!
WEMBE MIA TU!
UKININUNULIA "KASTALETI" UMENIMALIZA
HIZI NI ZAMA ZA "MADELA" SIO MAGARI.
NITAKUTUMBUA KABLA SIJATUMBU-LIWA, LETE WAGENI WANIONE.
MLANGO UPO WAZI WANAKUONA
TUKUTANE BAR JIONI.
UNAOTA?
NINGESHINDA SAA HIZI NA MIMI NAISHI ROHO INA-NING'INIA KAMA POPO!
WE' POKEA NDIO HALI HALISI.
"BUKU?"

## HABARI KIMATAIFA

# Wapalestina 90 wauawa kwenye shambulizi Gaza

**GAZA,** PALESTINA

KUNA hali ya kuogofya Ukanda wa Gaza, baada ya jeshi la Israel kufanya shambulizi baya katika shule moja na kuua watu zaidi ya 90.

Tukio hilo lilitokea jana na kusababisha vyombo vya habari kutofautiana idadi kamili ya watu waliokufa, huku Shirika la Ulinzi wa kiraia la Gaza ,linalosimamiwa na kundi la Hamas linaeleza watu 90 na mengine yakidai inafikia 100.

Shambulio hilo limeikumba shule ya "Al-Tabai' een, katika eneo la Al-Sahaba katika Jiji la Gaza.

Msemaji wa shirika la ulinzi wa kiraia, Mahmoud Bassal aliliambia shirika la habari la AFPm, kuwa eneo hilo lilikuwa wakiishi Wapalestina walikimbia makazi yao limeshambuliwa na mabomu matatu.

Alielezea mauaji hayo kuwa ya kikatili na imeacha miili ikiteketea kwa moto.

Shule ya Al-Tabi'een ni mojawapo ya makazi yaliyoko katikati mwa Jiji la Gaza, ambayo inawapa hifadhi watu 250 waliokimbia makazi yao.

Kulingana na vyombo vya habari vya Hamas, zaidi ya nusu ya watu wanaoishi hapo ni watoto na wanawake.

Jeshi la Israel, kwa upande wake, linadai kuwa limewapiga kwa usahihi magaidi wa Hamas ambao wanafanya kazi ndani ya kituo cha kijeshi cha Hamas kilichopo katika shule ya Al-Tabai'een.

Ilisema kituo hicho kinatumika kama maficho ya magaidi na makamanda wa Hamas.

Ijumaa jeshi la Israel lilitangaza kuwa lilikuwa linajihusisha na mapigano ya ardhini na kwenye mahandaki katika eneo la Khan Younes, jiji kubwa lililoko kusini mwa Gaza ambalo limegeuzwa magofu.

Mashambulizi hayo ya anga yalilenga zaidi ya maeneo 30 ya Hamas.

Ofisi ya Kuratibu masuala ya kibinadamu na misaada ya dharura (OCHA) ilikadiria kuwa Wapalestina 60,000 wamehamia magharibi mwa Khan Younes katika muda wa saa 72 zilizopita.

Uhamaji huo unatokana na maagizo ya kuondoka kaskazini mwa eneo hilo.

Awamu tofauti za vita vilivyoanzishwa na Israel katika Ukanda wa Gaza inasababisha kuhama mara kwa mara kwa watu masikini ambao wako hatarini.

Shule, ambazo huhifadhi watu waliokimbia makazi yao, mara nyingi hulengwa na jeshi la Israel kama shule ya al-Awda iliyoko Abassan, Khadija ya Deir al-Balah na shule ya UNRWA iliyoko Nouseirat.

Wakati huohuo, nchi hizo tatu za upatanishi, Qatar, Marekani na Misri zilitoa wito wa kuanza tena mazungumzo Agosti 15, kwa majadiliano yasiyo ya moja kwa moja kwa nia ya kusitisha mapigano.

**RFI**



Wakazi wa Goma wakitumia mitumbwi kukimbia mapigano yanayofanywa na waasi wa M23 katika eneo la Rutshuru jana. **PICHA: AFP**

# Ajali ya ndege yaua 62 Brazil

**SAO PAULO,** BRAZIL

WATU 62 wamekufa baada ya ndege inayomilikiwa na shirika la Voepass kuanguka na kuwaka moto katika jimbo la Sao Paulo nchini Brazil.

Ndege hiyo ilikuwa ikisafiri kutoka Cascavel, katika jimbo la kusini la Parana, kuelekea Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Guarulhos huko Sao Paulo, ilianguka katika mji wa Vinhedo, kulingana na vyombo vya habari vya ndani.

Hakuna ripoti rasmi iliyotolewa kuhusu ndege hiyo yenye chapa ATR-72 iliyokuwa imebeba abiria 58 na wafanyakazi wanne.

Rais wa Brazil, Luiz Lula da Silva, alisema inaonekana kwamba watu wote wameangamia, lakini hakutoa uthibitisho.

"Ndege imeanguka hivi punde kwenye mji wa Vinhedo, katika jimbo la Sao Paulo, ikiwa na abiria 58 na wafanyakazi wanne na inaonekana wote wamekufa," alisema Ras Lula na alikaa kimya kwa dakika moja kwa heshima ya watu waliokufa.

Mamlaka ya Valinhos, ilisema hakuna manusura na kwamba ndege hiyo iliyoanguka karibu na jengo la makazi, iliharibu nyumba moja pekee.

Hata hivyo, hakuna raia wanaoishi hapo aliyejeruhiwa.

Katika taarifa kwa vyombo vya habari, shirika la Voepass iliripoti tukio hilo la ajali ya ndege yenye namba 2283 katika eneo la Vinhedo.

"Ndege ilipaa kutoka Cascavel kuelekea Guarulhos, bado hakuna uthibitisho kuhusu mazingira ya ajali na hali ya sasa ya watu waliokuwamo," ilisema taarifa ya kampuni hiyo.

Ndege hiyo yenye chapa ATR 72-500, ilitengenezwa nchini Ufaransa.

Mji wa Vinhedo, wenye wakazi wapatao 76,000, uko kilomita 80 kaskazini-magharibi mwa Sao Paulo.

Picha zilizorushwa na vyombo vya habari vya ndani zinaonesha ndege hiyo ikianguka kwa mwendo wa kasi, na nyingine zikionesha moshi ukipanda juu ya eneo lililoonekana kama makazi ya watu.

Vikosi vya wazima moto, polisi wa kijeshi na walinzi wa raia wamepelekwa katika eneo hilo kwa ajili ya uokoaji.

**RFI**

# Kiongozi mpya Bangladesh ahubiri amani za dini zote

**DHAKAR**, BANGLADESH

KIONGOZI wa Serikali ya mpito nchini Bangladesh, Muhammad Yunus, ametoa wito wa kuvumiliana katika masuala ya imani za kidini.

Kauli hiyo aliitoa jana wakati akimfariji mama aliyekuwa akimlilia mwanae baada ya kuuawa kwa kupigwa risasi wakati wa maandamano.

Mama huyo alihuzunishwa na kisa cha mwanawe Abu Sayeed, aliyeuwawa kwa kupigwa risasi katika maandamano yaliyohitimisha utawala wa miaka 15 wa Waziri Mkuu, Sheikh Hasina.

Yunus ambaye ni mshindi wa Tuzo ya amani ya Nobel, alirejea nchini humo kutoka barani Ulaya alikokuwa akiishi uhamishoni, kwa ajili ya kuiongoza nchi hiyo kuelekea mageuzi ya kidemokrasia.

Yunus alisema wajibu wake sasa ni kujenga Bangladesh mpya isiyokuwa na migawanyiko ya kidini

Kazi kubwa itakayomkabili kiongozi huyo ni kurejesha umoja na amani pamoja na kuingoza nchi hiyo kuandaa uchaguzi mpya baada ya kuondolewa kwa Hasina.

Hata hivyo mtoto wa kiume wa Hasina, Sajeeb Wazed alisema serikali iliyoko sasa sio halali.

Serikali ya Sheikh Hasina aliye na miaka 76 inashutumiwa kwa matukio ya ukiukwaji wa haki za binadamu ikiwemo mauaji ya kiholela ya maelfu ya wapinzani wake kisiasa. Sheikh Hasina alitoroka nchi hiyo na kukimbilia India.

**DW**

MAKALA

# ANZIA SOKONI KISHA MALIZIA SHAMBANI KWA KIPATO ZAIDI



Na Magabilo Masambu

Utafiti huu unaozungumzwa si wa chuo kikuu bali ni kazi rahisi tu. Mkulima atatembelea masoko yaliyo karibu yake ili kufahamu ni wakati gani zao fulani huwa linaadimika katika soko hilo, akishabaini ndipo anakwenda shambani kulima ili wakati anavuna, soko liwe lina uhitaji mkubwa wa zao hilo. Tafsiri yake bei itakuwa juu.

WASWAHILI wanasema mchuzi wa mbwa unanywewa angali wa moto. Hii ni kutokana na Maonesho ya kilimo na sherehe za Nanenane 2024, ambayo mwaka huu yalikuwa ya 30 tangu yalipoasisiwa mwaka 1994.

Sherehe hizi zimekuwa zikilenga kutambua na kuthamini mchango wa wakulima, wafugaji na wavuvi kama tunavyofahamu kuwa kilimo na ufugaji ndiyo msingi mkuu wa maendeleo ya sekta zingine na maendeleo ya taifa kwa ujumla.

Katika sherehe za mwaka huu, kuna jambo kubwa nimejifunza na nikaona ni vyema kuwashirikisha wakulima wetu nchi nzima, ili kulima kilimo cha tija na chenye kipato kikubwa badala ya kilimo cha mazoea cha miaka nenda rudi.

Katika sherehe hizo, nimepata nafasi ya kutembelea banda la kilimo la Halmashauri ya Arusha, kwanza nikazungumza na Mkuu wa Kitengo cha Kilimo, Bahati Mtweve, ambaye alinieleza jinsi mradi wa TANSHEP unavyotekelezwa katika kuwapa elimu ya kilimo biashara wakulima.

Anasema kwa miaka ya nyuma, wakulima walikuwa wanalima kwanza ndiyo wanakwenda kutafuta soko, hivyo matokeo yake walikuwa wanapata hasara lakini sasa wanafundishwa kwamba anzia sokoni na kumalizia shambani kwa kipato zaidi.

Katika hali ya kawaida, wakulima wengi nchini wamekuwa wakilima kilimo cha mazoea kwa maana ya kufuata msimu wa mvua pekee, bila kufahamu kwanza soko linataka nini.

Sasa jambo jipya nililojifunza ni kwamba ili wakulima walime kilimo chenye kipato kikubwa, kwanza hawana budi kufanya utafiti wa soko linahitaji nini kwa kipindi gani hasa kilimo cha mboga ambacho ni cha muda mfupi.

Utafiti huu unaozungumzwa si wa chuo kikuu bali ni kazi rahisi tu. Mkulima atatembelea masoko yaliyo karibu yake ili kufahamu ni wakati gani zao fulani huwa linaadimika katika soko hilo, akishabaini ndipo anakwenda shambani kulima ili wakati anavuna, soko liwe lina uhitaji mkubwa wa zao hilo. Tafsiri yake bei itakuwa juu.

Wakulima wengi wanalima mazao yenye kufanana kwa wakati mmoja, jambo linalofanya bei ya mazao kuwa chini kwa sababu wanakuwa wamezalisha wengi. Mfano, wanasema mwezi Februari ndiyo kilimo cha nyanya hukubali kwa hiyo, wanaingia shambani kwa fujo mwisho wa siku wanazalisha nyanya za kutosha na wanauza kwa bei ya chini kutokana na upatikanaji mkubwa.

Godfrey Logati, mmoja wa wakulima, anasema walipata mafunzo ya kufanya utafiti wa kuanzia sokoni kutafiti bei za mazao kwa msimu husika kabla ya kuamua kulima zao fulani.

Ndipo hali ya kilimo ilipoanza kubadilika na kuwa kilimo biashara na kwamba elimu hiyo imewafanya wakulima kulima kilimo cha kisasa kinachoendana na mahitaji ya soko na kuwaondoa kwenye kilimo cha mazoea cha kulima tu ilimradi umeotesha mazao shambani.

Lucy Mvungi ni Ofisa Kilimo cha Mboga na Matunda Halmashauri ya Arusha. Anaesema moja ya faida kubwa ya progamu ya anzia sokoni malizia shambani kwa kipato zaidi, imewaondoa madalali wa mazao kwa kiasi kikubwa ambao waliwanyonya wakulima kwa muda mefu.

Kwa sasa wakulima wanayo mawasiliano ya moja kwa moja na wafanyabiashara sokoni, hivyo mkulima anaamua amuuzie dalali ama kwenda sokoni moja kwa moja kwa kuzingatia bei halisi ya soko.

"Tunawafundisha wakulima kukokotoa hesabu zao kabla ya kufanya uamuzi wa kuuza. Kwa hiyo hata akiamua kumuuzia dalali hatauza kwa hasara kama ilivyokuwa awali, maana bei ya soko sasa anaijua", anasema.

Halmashauri ya Arusha imeshika nafasi ya tatu kwa Kanda ya Kaskazini kwenye upande wa kilimo mazao na moja ya sababu iliyoelezwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Sulemani Msumi, nje ya maandalizi mazuri na namna walivyojipanga ni pamoja na elimu ya kuanzia sokoni na kumalizia shambani, ambayo kwa kiasi kikubwa imewasaidia wakulima hasa wa mboga kuzalisha kwa tija na kulipamba banda hilo kwa mazao yenye afya.

Kwa mujibu wa Tovuti Kuu ya Serikali, sekta ya kilimo nchini ni mhimili wa maendeleo ya uchumi. Sekta hii inachangia nusu ya pato la taifa, robo tatu ya bidhaa zinauzwa nje ya nchi na chanzo cha chakula pamoja na utoaji wa fursa za ajira zaidi ya asilimia 75 ya Watanzania.

Kwa mantiki hiyo, kilimo kina uhusiano na sekta nyingine mfano usafirishaji kwenda kwenye usindikaji wa mazao ya kilimo. Inatoa malighafi kwa viwanda na soko kwa bidhaa zinazotengenezwa. Tanzania inazalisha takribani asilimia 97 ya mahitaji yake ya chakula. Uzalishaji wa mazao ya chakula unatofautiana mwaka hadi mwaka kutegemea kiasi cha mvua kinachopatikana.

***0689157789***
***magabilomjalifu@gmail.com***
***Arusha-Tanzania***

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Mke wa mwenzio usimvalie suti, tai, mume wa mwenzio usimpakie wanja*



Na Adam Fungamwango

"Mke wa mwenzio mwache apite zake, mke wa mwenzio mpe zake heshima, mke wa mwenzio usimkaribishe kwenye baa, mke wa mwenzio usimvalie koti, mke wa mwenzio usimfungie tai, kuna wengine wadada wanayo hiyo tabia mbaya. Mume wa mwenzio usimpakalie wanja, mume wa mwenzio usijipishepitishe, akikutongoza kataa, akizidi kukufuatafuata kamwambie mumewe."

MKE wa mtu ni sumu na mume wa mtu naye ni sumu pia. Huu ni msemo wa vijana wa kileo na wasanii wa bongo fleva wametunga nyimbo mbalimbali kuelekeza juu ya baadhi ya watu wasiokuwa na adabu wala heshima kutongoza wake au kuchukua waume za watu.

Hili jambo halikuanza leo. Liko tangu enzi na enzi, lakini ukweli unabaki pale pale kuwa ni jambo la hatari, ambalo linasababisha ndoa nyingi kuvunjika, ugonjwa wa sonona, wahusika kubaki vilema au vifo.

Mambo yote haya yanafanyika kwa baadhi ya watu ambao unaweza kusema hawana hofu ya Mungu. Yeyote mwenye hofu hiyo hawezi kufanya mambo ya kipuuzi kama hayo.

Wanawake wapo wengi ambao hawajaolewa na wanaume wengi ambao hawajaona, hawatoshi mpaka unakwenda kuchukua mke au mume wa mtu?

Hapo kuna vitu ambavyo nataka kuainisha ambavyo huwa vinatokea. Kwanza kabisa mwanamume anamtongoza mwanamke. Kwa nini anayetongozwa hakatai kuwa ameolewa? Na kuna wanaume ambao hata wakijua kuwa mwanamke anayemtaka kumbe ameolewa bado wanakuwa ving'ang'anizi. Hata kama mwanamke alidanganya kama hajaolewa na baadaye mwanamume ukajua kuwa umeongopewa kwa nini usimwache? Ni hatari kuendelea kuwa na mpenzi wa aina hiyo.

Kwanza, huna raha naye. Muda wote roho juu, na wasiwasi saa zote ya kuogopa kufumaniwa. Huinjoi kwa kwenda naye popote pale, sasa yote ya nini?

Wako kinadada hata akijua kuwa yule ni mume wa mwezake, iwe shoga yake au jirani, anajipitishapitisha, atamtega mwanaume wa watu mpaka akingie mtegoni. jambo hili si zuri hata kidogo. Ndiyo maana wanamuziki wa zamani walitunga nyimbo nyingi kulikemea.

Moja ya tungo safi kabisa ni kutoka kwa bendi ya Super Matimila, ikiwa na Dk. Remmy Ongalla, mwanzoni mwa miaka ya 1980 ILIifyatua kibao 'Natoa Onyo.' Kilikuwa Kinawaonya wale wenye tabia hizo. Haya ndiyo mashairi yake;-

"Bibi wa mwenzio usimuwekee, macho mia mia, gharama alizipata kwa yule bibi haujui ndugu. Ninakuonya, nakuonya usirudi tena, huyo mwenzako oo ni rafiki yako, mmezoena, ninakumba, nakuomba usurudie tena, huyo mwenzao oo ni rafiki yako, tumezoeana.

Kumbuka mmekaa wote siku nyingi na ndugu huyo, vituko vyake uache ndugu, mbele ya kipenzi cha mwenzio, si vizuri ndugu, lawama ya bure."

Hapa inaonekana Remmy anamwonya jamaa aliyekuwa ameanza kunyemelea mke wa rafiki yake halafu baada ya hapo anatoa onyo kwa wale wote wenye tabia hiyo, waume kwa wake.

"Natoa onyo kwako kama ndugu, tabia hiyo siyo nzuri oo duniani, usiwe na haraka ya maisha wee kaka, waliotangulia wako wapi hivi sasa.

Starehe hazina mwisho, mke wa mwenzio mpe zake heshima, mke wa mwenzio usimfuatefuate, mkuki mtamu kwa nguruwe, kwa binadamu mchungu."

Hapa anajaribu kumwambia yeyote mwenye tabia hiyo kuwa kama yeye ndiyo ana mke, halafu atafanyiwa hivyo, atajisikiaje, ndiyo maana ya methali hiyo, ambayo ni sawa tu na ile ya 'mtenda akitendewa, huhisi kaonewa.'

"Mke wa mwenzio mwache apite zake, mke wa mwenzio mpe zake heshima, mke wa mwenzio usimkaribishe kwenye baa, mke wa mwenzio usimvalie koti, mke wa mwenzio usimfungie tai, kuna wengine wadada wanayo hiyo tabia mbaya.

Mume wa mwenzio usimpakalie wanja, mume wa mwenzio usijipishepitishe, akikutongoza kataa, akizidi kukufuatafuata kamwambie mumewe."

Haya ndiyo maneno ya Dk. Remmy Ongalla katika kibao chake hicho ambacho kilivuma sana, akiimba yeye mwenyewe, Skassy Kasambula na Kasaloo Kyanga katika mtindo wa Talakaka.

OTTU Jazz Band, wana wa Msondo Ngoma, mwanzoni mwa miaka ya 1990, walitunga kibao kiitwacho,'Usiendekeze Moyo' utunzi wake Tx Moshi William, ambao maudhui yake yanafanana na hayo.

Moja ya vipande vya wimbo huo ninasema. "Usiendekeze moyo utakavyokutuma, unadanganya jaribu kushinda, usiposhinda, huna budi kuumia, utajifisha kitanzi pasipo huruma.

"Kumpenda mke wa rafiki yako mpenzi ni hatari, vipo vitu vya kupenda lakini vingine nina madhara, oo moyo utakupeleka kaburini." Ujumbe unaeleweka vizuri tu. Mwenye masikio ya kusikia na asikie.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

# Aka Simtaki-6

BAADA ya kumaliza masomo yake ya kidato nne na kushindwa kuendelea na masomo kutokana na hali duni ya wazazi wake, Shani alitakiwa kuolewa. Akakubali, lakini ni kwa yule ambaye anampenda. Haikuwa hivyo, kwani baba yake mzee Chilambo alimlazimisha aolewe na mwanamume mwenye uwezo, mali na fedha ili asiende kuteseka. Tatizo likaanzia hapo, mwenye pesa hakupendwa na Shani, asiye na uwezo alikuwa kwenye moyo wake. Baba anamtaka mwenye uwezo. Jambo hili linazua mgogoro mkubwa kwenye familia tatu, za binti na wachumba wawili. Nini kitatokea. Usikose kila nakala ya gazeti hili.

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

NDIYO ni mzee kutoka kijiji cha jirani, Mtapenda, huyo mzee ana kijana wake anaitwa Fotu, ndiyo anataka kukuoa na yeye ndiye aliyefuzu vigezo vya kukuoa."

Maneno hayo yalimchanganya Shani. Alichojua ni kwamba mama yake angefikisha ujumbe kwa waliokuwa wanachuja hizo barua mbili na kubaki na yule anayempenda tu. "Hapana baba." Akajibu lakini kwa sauti ya chini ya woga. "Unasemaje?" Baba akahoji. "Baba nadhani barua ambayo ningependa ikubaliwe ni ile mliyoiacha." Macho yalimtoka pima mzee Chilambo. Alionekana kuwa na hasira ambazo zilimfanya ashindwe kuongea. "Mwanangu, kwa nini unakataa bahati hii?" Bi Hanifa alionekana kusikitika. Shani akaonekana kumshangaa mama yake. Alionekana kubadilika. Awali alionekana kama yupo naye na akamkabidhi kazi ya kuwashawishi barua anayoitaka ipitishwe. Aliona amesalitiwa. Na hilo lilionekana kumsikitisha sana. Asichokijua ni kwamba mama yake alifanya kila njia lakini ikashindikana. Ilikuwa nusura achezee kichapo kutoka kwa mumewe. Siku tatu baadaye akaletewa pesa kiasi cha shilingi elfu kumi ambacho hakikuwa kwenye mahesabu yoyote wa posa wala nini. Akaona bure awe upande huo huo. Ukinshindwa adui yako ni bora kuungana naye. Ndivyo alivyoona. "Unasikia, ukoo ambao unataka kumuoa una uwezo mkubwa, hii barua tu imewekwa elfu thelathini, uliona wapi hii, usiipoteze binti." Mshenga akasaidia. "Nimesema 'aka huyo mchumba simtaki."

*********************************

"Kwa nini wazazi wako wamekataa posa yangu?" "Sijui, mimi sikuwepo hapa, kama unavyojua nilikwenda kwa shangazi nikakaa kwa wiki mbili, huku nikowaacha wakafanya hivi walivyofanya"

Shukuru na Shani waliulizana na kujibizana walipokutana katikati ya njia inayogawa mpaka wa kijiji chao na Lalanguru na Mtapenda. "Ila mpenzi wangu kuwa mpole, usijali, niachie mimi hilo..!" "Nisijali nini wakati baba yako ameshakataa posa yangu?" "Sikiliza nikwambie Shukuru, hivi ninavyokwambia nikataa barua ya mchumba mwingine iliyoletwa nyumbani." Kuwepo kwa barua nyingine zaidi ya ile aliyopeleka yeye kulimshtua sana Shukuru. "Eee, unasemaje?" "Shukuru mpenzi wangu nikwambie kuna vita kubwa sana. Kulikuwa na barua mbili nyumbani, moja ya kwako na nyingine inasemekana imetoka kijiji jirani cha Mtapenda, lakini nimeikataa." Shani akajibu. "Lakini ya kwangu pia imekataliwa." "Kwanza waliikataa ya kwako, wakaipitisha ya huyo mwanaume mwingine sijui nani toba, ilikuwa na pesa sijui elfu thelathini, sijui hamsini, lakini nikakataa katakata." "Sina tatizo na wewe Shani, ila tatizo lipo kwa wazazi wako, sana sana baba yako. Nilikwambia haya mambo ya kuleta barua hivi sasa yasimame kwanza, nitafute kazi au vibarua nipate pesa ndiyo nije, vinginevyo ninadhalilika kwa sababu baba yako anapenda sana watu wenye uwezo."




**"Si hivyo Shani, kama kuna watu ambao wameshaleta barua kwenu na wazazi wako wameikubali na ya kwangu wameipiga chini, wewe si wa kwangu tena." Akasema Shukuru kwa uchungu.**

"Hapana Shukuru, usijali mimi nitasimama kidete, sitokubali la mtu yoyote." "Si hivyo Shani, kama kuna watu ambao wameshaleta barua kwenu na wazazi wako wameikubali na ya kwangu wameipiga chini, wewe si wa kwangu tena." Akasema Shukuru kwa uchungu. Ilionekana kama anataka kulia. Akainamisha kichwa chini. Shani akamshika begani ikiwa ni ishara ya kumbembeleza na kumtaka asikate tamaa. "Siyo hivyo mpenzi wangu." Akajaribu kumtuliza. Lakini Shukuru alionekana kuvunjika moyo. Mwili, na uso wake ulionekana vyema machochi mwa Shani kuwa amekata tamaa kabisa.

"Sikiliza nikwambie Shukuru, usikate tamaa, ninayeolewa ni mimi, hakuna wa kunilazimisha, mimi nimeshawaambia kuwa simtaki huyo wanayemtaka wao, enhee nimekumbuka, jina lake nimeambiwa ni Fotu, kutoka kijiji hiki kinachofuata cha Mtapenda, halafu baba yake ana uwezo, wanasema mzee Kandege sijui nani..." "Ahaaa, nishamjua, huyo ni mzee Kibopa, ndiye tajiri wa kijiji cha Mtapenda. Hilo Kibopa ni jina la utani, jina lake halisi ndiyo hilo Kandege." "Basi kama ndiyo huyo nimeshamsikia, mimi namjua kwa jina la mzee Kibopa, lakini pale walisema mzee Kandege, sasa mtoto wake ndiyo huyo aliyeleta barua." Shani akaendelea kutanabaisha. Taarifa kuwa aliyeleta barua kumbe ni mtoto wa mzee Kibopa, ikaendelea kumtisha Shukuru. "Usijali mpenzi, mimi niko upande wako." Shani alimsisitizia Shukuru.

********************************

"Mwanangu kwa nini hutaki kunisikia? Kwa nini hutaki kuolewa na Fotu?" "Baba mimi mchumba niliyemchagua ni Shukuru peke yake." "Kwa nini hutaki kuolewa na Fotu? Akarudia swali mzee Chilambo.

"Aka Simtaki." Akajibu. Mzee Chilambo alikuwa ameitisha kikao kwa ajili ya kushinikiza binti yake akubali kuolewa na mtoto wa Kibopa. Kilikuwa ni cha watu watatu, yeye, mkewe na Shani mwenyewe.

"Hivi wewe mwanangu umelogwa?" Akaongea kwa upole ambavyo si kawaida yake. Ilionekana kama ni njia ya kumbembeleza. Halafu akaendelea.

"Mbona unataka kufifisha bahati yako? We unaona huyo mtu wako kaweka shilingi elfu tano tu kwenye barua ya posa, lakini iliyotoka Mtapenda ilikuwa na shilingi elfu thelathini." "Unajua baba, ingawa huyo kijana mwingine sijawahi kumuona, lakini sijampenda, mimi namtaka Shukuru tu." "Mimi nadhani labda tumwite basi ili umuone, unaweza kubadili mawazo yako."

Wakati huo wote, Bi Hanifa alikuwa kimya akimsikiliza mumewe na binti yake wakilumbana.

"Unasikia mwanangu, Fotu ni kijana mtanashati, anavyovyaa mwenyewe utapenda, pili ni msomi, unajua msomi ni msomi tu hata mawazo yake ya kisomisomi, nne anatoka kwenye familia yenye uwezo, hivi unataka mwanangu ikitoka hapa msichana mzuri tu, halafu ukifika huko uwe kama bibi kizee." Pamoja na maneno yote hayo, hayakubadilisha msimamo wa Shani. "Baba, mimi Shukuru ndiye mwanaume wangu wa maisha, wala si mwingine."

Mzee Chilambo alionekana kubadilika. Hasira ilijidhihirisha machoni mwake. Akaona akiongea amekaa hatosikika. Akasimama na kuanza kupayuka "We mtoto, mimi baba yako au siyo baba yako? Nimbie ukweli leo, labda mama yako amekwambia kuwa mimi si baba yako?" Akauliza kwa sauti kali na ya kitisho.

"Baba yangu." Akajibu Shani kwa sauti ndogo na ya woga. "Sasa kama mama yako kakwambia mimi ndiyo baba yako kwa nini hutaki kunisikia ninavyosema. Angalia, nyumba yetu ni ya udongo hii, japo ni ya bati, lakini unadhani ukiolewa sisi hatuwezi kujengewa nyumba ya matofali hapa? Tutakaa hivi mpaka lini?"

Shani hakujibu lolote, akaanza kutokwa machozi. Hayakumzuia mzee Chilambo kuendelea kufoka.

"We mtoto, unasema unampenda sana Shukuru wako huyo. Una kichaa. Siku hizi kuna mapenzi! Yaliondoka tangu enzi za nabii Nuhu na Safina yake. Siku hizi watu wanaangalia fursa! Wanakwenda kuishi sehemu ambayo anaona atafaidika, ataheshimika na kuonekana mtu mbele za watu. Hawabebwi tena na hisia za mapenzi.

Hayo yaliwachelewesha hata bibi zetu enzi hizo. Siku hizi wanawake wanajitambua. Siyo kama wewe." Mzee Chilambo akazidi kubwata. Maneno hayo yalisababisha mkewe aingilie kati. "Basi baba Shani, usimwambie hivyo mtoto." "Nakwambia, nitawavuruga wote nyinyi wote wawili mtu na mama yake." Akasema huku akiwasogelea.

**Itaendelea Jumapili**



# USIYOYAJUA KUHUSU KOMASAVA

BAADA ya wimbo wa Komasava wa mwanamuziki maarufu wa Bongo Fleva, Diamond Platnumz, kuendelea kufanya vizuri, mwongozaji wa video ya wimbo huo Majagi King amesema kazi yote imefanywa na mdogo wake Fole-X.

Akizungumza na EATV, Majagi amesema kwamba kuna watu wengi nyuma yake na kwamba watu wasiojua ni kuwa video hiyo ambayo imeishtua dunia wazo lake lilitolewa na kijana huyo ambaye wanafanya kazi pamoja.

"Mwongozaji wa video ile ni Fole X, yeye ndiyo katoa wazo na tukaanza kulifanyia kazi. Sisi kama timu tulikuwa tunatengeneza kutokana na mwogozo wa falsafa na ubunifu wake na sisi wengine tulimsaidia," amesema Majagi.

EATV

# RICH MAVOKO ALIKATAA KWENDA WCB

BAADA ya bifu la muda mrefu kati ya mwanamuziki Rich Mavoko na iliyokuwa lebo yake WCB, kumeibuliwa tuhuma kuwa kulikuwa na vita hadi msanii huyo kujiunga nao.

Akizungumza hivi karibuni, Prodyuza maarufu Mazuu, amesema ni wao ndiyo walilazimisha aende kwao, kwa sababu alikuwa ni mtoto msumbufu kuliko AliKiba.

"Kipindi hicho Rich Mavoko ana wimbo mkubwa kuliko Diamond, walimpa machaguo mawili kama anataka kuendelea na muziki aende WCB kama hataki abaki huko huko, mimi ikabidi nikate tamaa kwa sababu vita ya WCB ilikuwa kubwa na Rich Mavoko alikuwa amekataa kabisa kujiunga WCB ikabidi nimuombe" amesema Mazuu.

## ZISIKUPITE

**BERGE ATAKIWA MAN UNITED**
KLABU ya Manchester United inaweza kumjaribu kiungo wa kati wa Burnley na Norway, Sander Berge mwenye umri wa miaka 26, kwenda Old Trafford kwa kumpa mkataba wa kulipwa mshahara wa pauni 100,000 kwa wiki. (**Sun**)

**TRIPPIER ATAKIWA WEST HAM**
WEST Ham inavutiwa na beki wa kulia wa England, Kieran Trippier, huku mustakabali wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33 huko Newcastle United bado haujaamuliwa. (**Telegraph**)

**OMORODION SAFI CHELSEA**
CHELSEA imekubali mkataba wa pauni milioni 35 na Atletico Madrid ili kumsajili mshambuliaji wa Hispania, Samu Omorodion, na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20 anatazamiwa kufanyiwa uchunguzi wa kimatibabu. (**Fabrizio Romano**)

**ZUBIMENDI KUTUA LIVERPOOL**
KIUNGO wa kati wa Hispania, Martin Zubimendi anatarajiwa na Real Sociedad kukubali kuhamia Liverpool, ingawa klabu hizo bado zinahitaji kuafikiana dili la mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25. (**Athletic**)

**BROJA KUAMUA HATIMA**
MSHAMBULIAJI wa Chelsea na Albania, Armando Broja atafanya mazungumzo na kocha, Enzo Maresca kufahamu mustakabali wake. Everton na Wolves ni miongoni mwa timu zinazomtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22. (**Mail**)

**CHALOBAH AIVUTIA W'HAM**
WEST Ham inavutiwa na mlinzi wa Chelsea, Trevoh Chalobah mwenye umri wa miaka 26, na beki wa kati wa Ujerumani, Mats Hummels mwenye umri wa miaka 35, ambaye ni mchezaji huru baada ya kuondoka Borussia Dortmund. (**Sky Sports**)

**CRYSTAL PALACE PIA INAMTAKA**
KLABU ya Crystal Palace pia inamtazama mlinzi wa Chelsea, Trevoh Chalobah, na mlinzi wa Wolfsburg ya Ufaransa, Maxence Lacroix mwenye umri wa miaka 24, kama chaguo la beki wa kati. (**Telegraph**)

**CASTLEDINE ATAKIWA CHELSEA**
CHELSEA imewasiliana na Rangers kuhusu uwezekano wa kumnunua kiungo wa kati wa akademi mwenye umri wa miaka 19, Leo Castledine. Aberdeen pia inavutiwa na mwingereza huyo. (**FootballScotland**)

**LIVERPOOL YAMGANDA BEIER**
LIVERPOOL bado inavutiwa na mshambuliaji wa Ujerumani na Hoffenheim, Maximilian Beier, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 anataka kujiunga na Borussia Dortmund na yuko kwenye mazungumzo na klabu hiyo ya Bundesliga. (**Sky Germany**)

**BELLA-KOTCHAP AKATALIWA**
KLABU ya Southampton imepokea ofa kutoka Hoffenheim kwa mlinzi wa miaka 22, Armel Bella-Kotchap. The Saints hao tayari wamekataa ofa ya pauni milioni 8.6 kutoka Stuttgart. (**Sky Germany**)

**DIGNE HAITAKI GALATASARAY**
MLINZI wa Aston Villa, Lucas Digne amekataa pendekezo la kujiunga na Galatasaray. Mfaransa huyo mwenye umri wa miaka 31 anatarajiwa kubaki na Villa. (**Athletic**)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# DE GEA ATUA FIORENTINA

**ROME,** Italia

**Golikipa huyo wa zamani wa Manchester United ameweka wazi kuwa mkataba wake ni...**

GOLIKIPA wa zamani wa Manchester United, David de Gea amejiunga na Fiorentina kama mchezaji huru, timu hiyo ya Serie A ilitangaza jana

De Gea mwenye umri wa miaka 33, ameweka bayana juu ya mkataba wa mwaka mmoja, na chaguo la kuongeza kwa msimu mmoja zaidi.

Mchezaji huyo wa zamani wa kimataifa wa Hispania amekuwa hana klabu tangu alipoondoka United majira ya joto yaliyopita.

De Gea alikuwa amepewa nyongeza ya mkataba mpya wa kuendelea Old Trafford lakini akachagua kumaliza miaka 12 katika klabu hiyo.

Tangu wakati huo, mchezaji huyo wa zamani wa Atlético Madrid amepokea ofa nyingi kutoka kwa klabu za Ulaya na Saudi Aarabia.

Alivutiwa na Genoa kabla ya hatimaye kuchagua kujiunga na Fiorentina, ambayo ilimaliza katika nafasi ya nane kwenye Serie A msimu uliopita.

De Gea alicheza mechi 545 akiwa na United na alikuwa sehemu ya timu iliyoshinda taji la Ligi Kuu England mwaka 2013 chini ya Sir Alex Ferguson.

Wakati akiwa Old Trafford, alishinda pia Kombe la FA, Ligi ya Europa na mataji mawili ya Carabao.

Fiorentina, ambao walisema De Gea atatangazwa kwa vyombo vya habari vya Italia kesho, walimaliza katika nafasi ya nane kwenye Serie A msimu uliopita na wanakabiliwa na mchujo wa kufika hatua ya tatu ya Ligi Uefa Conference.

# BARCELONA YAMSAJILI RASMI DANI OLMO



**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA imekamilisha usajili wa mshambuliaji wa RB Leipzig, Dani Olmo, klabu hiyo ya Katalunya ilithibitisha jana.

Vyanzo vimeiambia ESPN kwamba mpango huo una thamani ya euro milioni 55 na nyongeza ya euro milioni saba.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania ametia Saini mkataba wa miaka sita katika klabu hiyo hadi Juni 2030, na kipengele cha kutolewa kikiwekwa kuwa euro milioni 500.

"Nataka sana kuanza. Siku hizi zimekuwa kali, lakini kila kitu kilifanyika kwa kasi na nitaendelea kuwashukuru Leipzig," alisema Olmo akiwaambia waandishi wa habari.

"Tunaipa kila kitu tulicho nacho katika hatua hii mpya."

Olmo, ambaye alikuwa kwenye vitabu vya Barca hadi alipoondoka kwenda Croatia akiwa na umri wa miaka 16, anakuwa mchezaji wa kwanza kusajiliwa na klabu hiyo msimu huu wa majira ya joto huku wakiendelea kukabiliana na vikwazo vya kifedha vilivyowekwa na ukomo wa matumizi wa LaLiga.

Barca iliongeza mazungumzo ya kutaka kumsajili Olmo wiki iliyopita baada ya kukatishwa tamaa katika jitihada zao za kumsajili Nico Williams wa Athletic Club.

Mkurugenzi wa michezo Deco alisafiri kwa ndege hadi Leipzig mapema wiki hii, ambapo mazungumzo na kambi ya mchezaji na klabu ya Bundesliga yalizaa makubaliano kimsingi Jumanne.

Olmo mwenye miaka 26, alisafiri kwa ndege hadi Barcelona, uhamisho huo ukithibitishwa Ijumaa.

Vyanzo vya habari vinasema kusajiliwa kwa Olmo hakuondoi jaribio jipya la Williams kabla ya dirisha la uhamisho kufungwa mwezi huu, ingawa bado kuna kukubalika kwamba usajili wa winga huyo bado ni mgumu.

Baada ya kujiunga na akademi ya Barca ya La Masia kutoka kwa wapinzani wa ndani Espanyol mwaka wa 2007, Olmo aliondoka kwenda Dinamo Zagreb mwaka wa 2014 kutafuta njia ya haraka ya kucheza katika kikosi cha kwanza.

Alicheza mechi 124 kwa timu hiyo ya Croatia kabla ya kusajiliwa Leipzig mwaka 2020, ambapo alishinda DFB-Pokals mbili na DFL-Supercup, akifunga 'hat trick' katika fainali mwaka jana katika ushindi wa 3-0 dhidi ya Bayern Munich.

"Klabu changa, mchezaji mchanga ...., tulishinda mataji yetu ya kwanza na tukaweka historia pamoja," alisema Olmo kupitia kwenye Instagram, akitangaza kuondoka kwake Leipzig.

"Mataji mawili na Super Cup ni baadhi tu ya nyakati nyingi zisizoweza kusahaulika ambazo daima zitabaki nami. Asante RB Leipzig, utakuwa moyoni mwangu milele."

Olmo pia ameichezea Hispania na alichukua jukumu kubwa katika kampeni yao ya ushindi wa ubingwa wa Ulaya msimu huu wa majira ya joto, akifunga mara tatu na kutoa asisti mbili katika mechi zake sita.

# Guardiola: Hatukuweza kumzuia Alvarez

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola amesema Manchester City hawakuwa na chaguo ila kukubali ofa ya Atlético Madrid kwa ajili ya Julian Álvarez kwa sababu aliiambia klabu hiyo anataka kuondoka.



ESPN imeripoti kuwa Álvarez anakaribia kuhamia Atletico kwa ada ambayo inaweza kupanda hadi pauni milioni 82.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina amekuwa m muhimu katika uwanja wa Etihad kwa miaka miwili iliyopita, lakini Guardiola alisema klabu hiyo haikuwa katika nafasi ya kuzuia mpango huo.

"Sipendi kuwaambia wachezaji kile wanachopaswa kufanya," alisema Guardiola akiwaambia wanahabari siku ya Ijumaa.

"Mikataba ni mizuri lakini inaweza kuvunjwa, kama huna furaha kwa nini uwe hapa?

"Anapendwa sana na timu kwa tabia yake, lakini kama nilivyosema mara nyingi kwa wachezaji, ikiwa anataka kuondoka na anataka changamoto mpya, Atlético ni klabu kubwa nchini Hispania na Ulaya na walipopendekeza mimi kupitia klabu ambayo alitaka kuondoka, nilisema ni sawa fikiria anabaki wakati hataki kubaki?

Álvarez amefunga mabao 36 katika michezo 103 tangu awasili kutoka River Plate mwaka 2022.

Ameshinda mataji mawili ya Ligi Kuu Englans, Ligi ya Mabingwa Ulaya na Kombe la FA wakati alipokuwa City, lakini Guardiola amependekeza kuwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 amekuwa na motisha ya kuondoka kwa sababu anataka kuanza mara nyingi zaidi.

"Sijui sababu kwa nini. Alisema anataka changamoto mpya na anahisi ni kile anachopaswa kufanya," alisema Guardiola.

"Msimu uliopita alicheza sana na katika baadhi ya nyakati alicheza na Erling Haaland, lakini ninaelewa katika nyakati muhimu labda alifikiri atacheza. Ninamheshimu sana."

Uamuzi wa Álvarez unawaacha City na Guardiola wakiwa na mkanganyiko kuhusu kuwekeza au kutowekeza fedha kwa mshambuliaji mwingine kabla ya tarehe ya mwisho ya usajili.

"Bado sijui," Guardiola alisema. "Tunazungumza kila siku na kuona nini kinatokea. Sijui bado. Inaweza kutokea lakini haikuweza kutokea."

# De la Fuente aipongeza Hispania kutwaa dhahabu Olimpiki

**PARIS,** Hispania

LUIZ de la Fuente kocha wa timu ya taifa ya wakubwa ya Hispania amesema soka la nchi yake linapaswa kuthaminiwa zaidi baada ya timu ya vijana chini ya umri wa miaka 23 kupata medali ya dhahabu katika fainali ya michuano ya Olimpiki dhidi ya Ufaransa juzi.

De la Fuente aliiongoza timu ya vijana chini ya umri wa miaka 23 miaka mitatu iliyopita katika kumaliza medali yao ya fedha kwenye Michezo ya Tokyo kabla ya kuteuliwa kuwa kocha mkuu wa timu ya taifa na kushinda ubingwa wa Ulaya mwezi uliopita.

Kocha huyo aliomba watu wathamini nishani ya dhahabu ambayo kikosi cha Santi Denia kilishinda mjini Paris, ikiwa ni mara ya kwanza kwa nchi hiyo tangu mwaka 1992, na kazi kubwa iliyoifanya kufuatia majira ya kiangazi ambapo timu ya Hispania chini ya umri wa miaka 19 pia ilitwaa ubingwa wa Ulaya.



Timu yao ya wanawake pia imepata mafanikio makubwa, ikishinda Kombe la Dunia la mwaka jana na Ligi ya Mataifa ya mwaka huu, ingawa walishindwa na Ujerumani katika mechi ya Ijumaa ya medali ya shaba.

"Hatujui tulichofanikiwa mwaka huu na hatuthamini soka la Hispania vya kutosha. Tuondoe chuki zetu, kwa kweli, karibu hakuna timu inayoweza kufikia hili," alisema De la Fuente akiwaambia waandishi wa habari.

"Pia timu ya vijana chini ya umri wa miaka 19, washindi wa pili wa Ulaya chini ya umri wa miaka 21 mwaka jana, tupe umuhimu kwa yale ambayo yamepatikana leo, huu ni usiku wa kihistoria, tumeishi hadithi kubwa ambayo itaingia kwenye historia ya Olimpiki na michezo ya Uhispania."

Kocha huyo mwenye umri wa miaka 63 pia aliwasifu Fermín López na Álex Baena ambao walikuwa sehemu ya kikosi chake kwenye michuano ya Euro kabla ya kujiunga na timu ya Olimpiki mwezi uliopita.

Taji la kandanda la Olimpiki pia linawakilisha medali ya kwanza ya dhahabu katika mchezo wa timu kwa Uhispania katika miaka 28.

## HABARI MICHEZO

# SIMBA YASAKA MSHAMBULIAJI

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya mechi ya nusu fainali ya Ngao ya Jamii dhidi ya Yanga na kuchapwa bao 1-0, viongozi wa Simba na Kocha Mkuu, Fadlu David wameonesha kutoridhishwa na safu ya ushambuliaji, hivyo wameamua kutafuta mshambuliaji mwingine kabla ya dirisha kubwa la usajili kufungwa, Agosti 15.

Benchi la ufundi linataka mshambuliaji mpya atakayekuja kusaidiana na Steve Mukwala huku Fred Michael akipewa nafasi ndogo ya kuanza kwenye kikosi cha kwanza.

**Habari kutoka ndani ya klabu hiyo zinasema viongozi wote wa Simba, akiwemo Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi, Mohamed Dewji, wamekubaliana kuwa wanahitaji mshambuliaji mpya haraka iwezekanavyo.**

Mtoa taarifa alisema kutokana na jinsi walivyoiona mechi hiyo, kama timu ingekuwa na mshambuliaji bora ingeweza kupata bao, lakini hakukuwa na kashikashi zozote langoni mwa Yanga, licha ya kiwango bora walichokionesha Simba.

"Wote wamekubaliana kuwa timu ni nzuri, lakini inakosa straika mwenye uchu wa mabao, na sasa tayari wameshaingia sokoni kumsaka mchezaji wa aina hiyo ambaye atatangazwa kabla ya dirisha dogo kumalizika, kwa maana hiyo kuna mchezaji mmoja ataondoka kumpisha, anaweza kuwa Ayoub Lakred, au Fred Michael," alisema mtoa taarifa huyo.

Hata hivyo mtoa taarifa huyo amesema kuna majina kadhaa ya wachezaji ambayo viongozi wanayo mkononi, lakini hajabahatika kuyaona na kuomba apewe muda.

"Kwa sasa sina majina ya wachezaji hao, ila nipe muda wa siku mbili tatu nitakupenyezea," alisema mtoa taarifa huyo.

Hata kwenye mechi tatu za kirafiki ilizokuwa ikicheza nchini Misri, Fadlu alikuwa akilalamikia safu yake ya ushambuliaji, akisema zinatengenezwa nafasi nyingi, lakini hazitumiwi.

Juzi baada ya mechi dhidi ya Yanga, alikiri kuwa bado kuna tatizo katika safu yake ya ushambuliaji na atalifanyia kazi kabla ya Ligi Kuu kuanza.

Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa Klabu hiyo, Crescentius Magori, alisema bado hawajamaliza kusajili mpaka dirisha litakapofungwa, lakini kabla ya hapo wanachama na mashabiki wategemee chochote kutokea.

SOKA



Mchezaji wa timu ya Videte Center, Michael John (katikati), akimiliki mpira huku akizongwa na wachezaji wa timu ya Maginja FC kwenye mchezo wa kirafiki uwanja wa kituo cha michezo cha Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Sababu dabi, Simba, Yanga kutokuwa na VAR hizi hapa

INATOKA UK. 24

mpaka wenyewe waje kujiridhisha kuwa wameiva kuwa sehemu ya VAR, baada ya hapo sasa tutaomba kibali cha kuitumia kwenye Ligi yetu," alisema Kasongo na kuongeza.

"Kwa hiyo, michezo ya awali hatutokuwa na VAR mpaka mchakato huo umalizike," alisema.

Hivi karibuni, Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF), liliipa Shirikisho la Soka Tanzania mitambo ya VAR, ambayo imefungwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, huku wadhamini waliopewa tenda ya kuonyesha mipira nao wakiahidi kuwa na VAR inayohamishika 'Mobile VAR.'

Baada ya mechi ya Alhamisi, ambayo Yanga ilishinda bao 1-0, baadhi ya mashabiki walilalamika kutotumika kwa VAR, na hiyo ilitokana na baadhi ya matukio tata ambayo mwamuzi Elly Sasii na wasaidizi wake walionekana kushindwa kuyaamua kwa usahihi.



# JWTZ waja na tamasha la Utamaduni

**Na Faustine Feliciane**

WAZIRI wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Damasi Ndumbaro anatarajiwa kuzindua mashindano ya kwanza ya Utamaduni ya Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi (CDF), Jenerali John Mkunda Agosti 19, mwaka huu jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Mwenyekiti wa Kamati ya mashindano hayo, Meja Jenerali Mbaraka Mkeremy, alisema mashindano hayo ni sehemu ya shamrashamra za maadhimisho ya miaka 60 ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ).

"Mashindano haya ni wazo la CDF, lengo lake ni kuhuisha sanaa na utamaduni nchini, akaona jeshi lina uwezo wa kufufua sanaa hiyo mpaka kufikia kimataifa, zamani wakati tuko shule ya msingi tulipata kuona sanaa mbalimbali ikiwamo mazingaombwe, sarakasi, ngoma za asili zetu na nyingine nyingi lakini sasa havipo tena.

"Kupitia mashindano haya kwa mara ya kwanza mwaka huu, yatashirikisha vikundi vya utamaduni na bendi za JWTZ, yataendelea kufanyika kila mwaka na 2025 tutaalika vyombo vingine vya ulinzi na usalama ikiwamo Jeshi la Magereza, Uhamiaji na Polisi pamoja na kuongeza fani nyingine za sanaa.

"Tunawaita Watanzania Wote waje kushuhudia burudani hizo zitakazozinduliwa hapa Msasani Klabu, hakutakuwa na kiingilio ni burudani kuelekea shamrashamra za miaka 60 ambazo kilele chake ni Septemba Mosi"alisema Meja Jenerali Mkeremy.

Meja Jenerali Mkeremy alisema Kamati yake itaundwa na majaji watatu kutoka Basata watakaoshauri na kuboresha mashindano hayo.

# Michezo

Jumapili Agosti 11, 2024

Nipashe



De Gea atua Fiorentina UK. 21



Feitoto

Aziz Ki

## Sababu dabi, Simba, Yanga kutokuwa na VAR hizi hapa

**Na Adam Fungamwango**

BODI ya Ligi imesema hakutakuwa na video ya kusaidia waamuzi VAR katika mechi za mwanzo wa Ligi Kuu mpaka hapo baadaye kutokana na marefa wanaotakiwa kufanya kazi hiyo kuwa kwenye mafunzo kwa sasa.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi hiyo, Almasi Kasongo, alisema hayo jijini Dar es Salaam, na kuzima malalamiko ya baadhi ya mashabiki wa soka nchini waliokuwa wanahoji kutokuwepo kwa VAR katika mchezo wa watani wa jadi, Simba na Yanga uliochezwa Alhamisi iliyopita, Uwanja wa Benjamin Mkapa, ikiwa ni nusu fainali ya Ngao ya Jamii.

"Kwa sasa tunawajengea uwezo waamuzi wetu wataokuwa kwenye VAR kama tulivyoelekezwa na CAF na FIFA, na watajifunza

INAENDELEA UK 23

# YANGA, AZAM FAINALI YA AINA YAKE LEO

## ●●●Gamondi afurahia mechi ngumu, Simba, Coastal Union kusaka nafasi ya tatu huku...

**Na Shufaa Lyimo**

WAKATI kocha wa Azam, Bruno Ferry akisema kikosi chake kipo tayari kuwakabili Yanga leo, kocha wa wapinzani wao hao, Miguel Gamondi, amesema anafurahia kukutana na mechi ngumu kwa kuwa inakifanya kikosi chake kuimarika zaidi.

Yanga na Azam zitakutana leo kwenye fainali ya Ngao ya Jamii kwenye mchezo utakaochezwa saa 1:00 usiku ukitanguliwa na mchezo wa kusaka nafasi ya tatu kati ya Simba na Coastal Union.

Yanga imetinga hatua hiyo baada ya kuifunga Simba bao 1-0 kwenye mchezo wa nusu fainali Alhamisi iliyopita huku Azam FC siku hiyo hiyo ikiiadhibu Coastal Union mabao 5-2 na kutinga fainali.

**Akizungumza na waandishi wa habari jana, Gamondi, alisema mchezo dhidi ya Simba na huu wa leo unakisaidia kikosi chake kuimarika kutokana na ugumu na ubora wa wapinzani wao.**

Alisema anatarajia kukutana na mchezo mgumu mbele ya Azam kwa wapinzani wao hao ni timu nzuri na anaiheshimu.

"Kwa upande wangu ninafurahi kukutana na timu yenye ushindani kama Azam FC kwa kuwa inakifanya kikosi changu kizidi kuwa bora zaidi, ninaomba mashabiki wetu waje kwa wingi uwanjani kuangalia burudani tutakayowapa," alisema Gamondi.

Alisema makosa madogo madogo aliyoyabaini katika mchezo wao wa nusu fainali dhidi ya Simba ameyafanyia kazi ili yasiweze kujirudia kwenye mchezo leo.

Kwa upande wake Dickson Job ambaye alizungumza kwa niaba ya wachezaji wenzake alisema mchezo huo utakuwa na upinzani kutokana na timu zote kuwa na mabenchi bora ya ufundi.

" Sisi wachezaji tunafahamu mchezo huo utakuwa mgumu hivyo tunaahidi kupambana ili tuweze kupata matokeo mazuri, alisema Job.

Kwa upande wake, Kocha wa Azam, Ferry alisema wanatarajia kupata ugumu mbele ya wapinzani wao kwa kuwa ni timu inayofanya vizuri kwa sasa.

"Mchezo utakuwa mgumu sitaki kuzungumzia Yanga kwa kuwa hakuna mtu asiyefahamu ubora wake, kikubwa ni kupata ushindi," alisema Ferry.

Alisema wamejiandaa na wapo tayari kukutana na yanga kwenye mchezo huo wa leo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >